epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US
Alhamisi Aprili 11, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0581643
www.ippmedia.com
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital



**'TUNAWEZA KUWAFUNGA CITY KWAO'**
UK.22

EID EL FITR

# Samia: Kuna mchezo mchafu kwenye kodi

• **Wamo** vigogo serikalini, atwisha mzigo Waislamu; mashekhe wahadharisha biashara ya dawa za kulevya, Katiba mpya nayo... *Endelea ukurasa 2 &3*

## Ajali ya basi ilivyoua tisa, kujeruhi 19

UKURASA 4



Rais Samia Suluhu Hassan akishiriki ibada ya Eid El Fitri katika Msikiti Mkuu wa Mfalme Mohammed VI wa Morocco, Kinondoni Dar es Salaam, jana. **PICHA: IKULU**



**Ukuta** wa uzio wa jirani waanguka na kuua baba, mwanawe

UKURASA 7



**Tume** ya Uchaguzi rasmi kuitwa Tume Huru ya Uchaguzi

UKURASA 19




**Mawakili** vitani kusaka vishoka wa mihuri yao

UKURASA 19




Basi la kampuni ya Lujiga Express lenye namba za usajili T 315 CXX likiwa limeligonga lori la mizigo lililokuwa limeegeshwa kutokana na kuharibika katika kijiji cha Malendi, wilayani Iramba mkoani Singida juzi alfajiri na kusababisha watu tisa kufariki dunia na wengine 19 kujeruhiwa. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

## Mafuriko Rufiji; timu mawaziri yaweka kambi

UKURASA 4

**MICHEZO** UCHOVU, UBUTU SIRI SIMBA KUBORONGA UK.24 **KATUNI** UK.6



Rais wa Zanzibar, Alhaj Dk. Hussein Ali Mwinyi akisalimiana na waumini wa kiislamu, baada ya swala ya Eid El Fitri katika Masjid Jamiu Zinjibar Mazizini, Wilaya ya Magharibi "B" Unguja jana. **PICHA: IKULU**

# Samia: Kuna mchezo mchafu mifumo kodi

**Na Romana Mallya**

RAIS Samia Suluhu Hassan amewalipua wafanyabiashara, watumishi wa serikali na waumini wa dini mbalimbali wanaochezea mifumo ya kodi kwa lengo la kujinufaisha na kuikosesha serikali mapato.

Kutokana na kuwapo tatizo hilo, Rais Samia amewatwisha jukumu viongozi na waumini wa dini ya Kiislamu kuisaidia katika kudhibiti uvujaji wa kodi na mapato ya serikali.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam katika Baraza la Eid-El-Fitr lililoandaliwa na Baraza Kuu la Waislam wa Tanzania (BAKWATA), Rais Samia alitaja mambo mawili likiwamo la umuhimu wa kodi akieleza kuwa ni kwa maendeleo ya taifa.

Rais Samia alikumbusha maneno yake aliyomweleza Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Alphayo Kidata, baada ya kumwapisha kuwa akakusanye kodi lakini zile za dhuluma hapana na kusisitizia suala la haki. Alisema kwa sasa ni miaka mitatu tangu amwapishe na bado anaendelea kusisitiza kodi za haki.

"Kwa sasa, makusanyo ya ndani yamepanda kutoka Sh. trilioni 18 mwaka 2020/21 hadi Sh. trilioni 24 mwaka 2022/23. Ninawapongeza wafanyabiashara wanaotoa risiti na wananchi wanaodai risiti," alisema.

Rais Samia alisema licha ya kupanda kwa mapato ya ndani, inasikitisha baadhi ya wafanyabiashara wanakimbia kulipa kodi, hawatoi risiti au wakitoa ni zenye upungufu na wanunuzi nao hawadai risiti.

"Ulipaji wa kodi ni halali kidini. Ni jukumu la kila mmoja wetu kupitia shughuli tunazofanya, kulipa kodi kwa haki na kuendana na sheria za nchi. Nilikataa kodi za dhuluma ili tuendane na misingi ya haki lakini inasikitisha kwamba wafanyabiashara wetu sasa wamegeuza.

"Tumekataa kodi za dhuluma kama serikali, wafanyabiashara wanafanya dhuluma ya kodi. Wanadhulumu kulipa kodi. Wanadhulumu mapato ambayo yangetumiwa kuhudumia wananchi .

"Pengine wanafanya hivyo kwa sababu mbalimbali, labda za kisiasa, kiuchumi ili wapate utajiri zaidi, wapate mapato mengi zaidi, au uhujumu wa makusudi kuendelea kuhujumu maendeleo ya wananchi," alisema.

Rais Samia aliwasihi waache dhuluma hiyo inayochelewesha maendeleo ya nchi na wote wawe raia wema na kutimiza wajibu wao.

### KIGOGO KATIKA MAGENDO

Rais Samia aliahidi kuendelea kusimamia haki kwenye ukusanyaji wa kodi, kuboresha mifumo na kuleta wepesi katika ulipaji na ukusanyaji wake na kuhakikisha inayokusanywa inatumika ipasavyo kwa manufaa ya wananchi.

"Imebidi nizungumze hili kwa kutumia jukwaa hili kwa sababu niwape hadithi, kule Zanzibar kulikuwa kumekithiri magendo ya karafuu. Wenye karafuu wanavusha wanazipeleka Mombasa (Kenya) na Mombasa zinakwenda mbele.

"Katika operesheni tuliyofanya, tukakuta kiongozi mkubwa serikalini yumo kwenye hilo jambo. Tulipomhoji kwa nini unafanya hivi, alisema "tumbo halina siasa, siasa ina kwake, lakini tumbo halina siasa, ndiyo iliyonipelekea kuvusha magendo hayo'.

"Na huyu ndiye tulimtegemea asimamie magendo yale yasifanyike. Nadhani kwa upande huu imenibidi niseme hapa kwa sababu kati yetu kuna wafanyabiashara wakubwa tu. Na dini yetu hii alhadullah Mungu ameturuzuku. Kuna wafanyabiashara wakubwa wenye imani yetu, lakini inasikitisha kwamba baadhi yao wana vipenyo vipenyo makusudi vya kukwepa kodi.

"Kama ni waumini wa dini basi warudi nyuma waone kwamba suala la kodi hata upande huu limehimizwa ni wajibu wao kulipa kodi kutokana na sheria za nchi," alisema.

Hata hivyo, Rais Samia alisema ni imani yake watamwelewa kwa kuwa wote wataelewana na watalipa kodi au watadai risiti kwa wafanyabiashara ili walipe kodi kwa wafanyabiashara ili serikali ifanye huduma kwa wananchi.

"Kuna mambo mengi, kuna mafuriko huko watu wanataka huduma, bila kodi huduma hizo zinakuwa hakuna. Nimeona nitumie Baraza hili nitoe ujumbe huu," alisema.

### SERA YA ELIMU

Rais Samia pia alisema maboresho ya sera ya elimu na mafunzo ya amali ambayo aliwaeleza, yamefanyika kwa lengo si tu kuhakikisha wanatoa elimu kwa wote, bali itakayowajengea vijana maadili na kutoa mchango kwa jamii katika mazingira ya sasa,

"Suala la elimu si la kufumbia macho ni imani yangu jukwaa hili ni muafaka kuzungumzia maboresho tuliyofanya kwenye mitaala na sera. Hali hii ilichangiwa na wategemezi katika jamii zetu. Serikali iliamua kupitia mapitio ya mitaala na sera mwaka jana.

"Kupitia sera hii tumeongeza msukumo kwenye elimu ya amali, tunatarajia mhitimu ataingia katika shughuli za uzalishaji mali mapema akiwa na stadi stahiki.

"Ninaomba ushirikiano wa taasisi za dini zenye shule na shule binafsi ziwe zinasadifu malengo ya sera. Kwa upande wa BAKWATA muimarishe shule zilizo chini yenu katika kutekeleza sera hii iliyoboreshwa, muwalee watoto wakiwa na elimu ya dunia na ya dini," alisema.

UCHAGUZI SERIKALI MITAA

Rais Samia alisema ni uchaguzi muhimu ambao unahusisha viongozi wanaokaa nao katika jamii zao na wamewahakikishia kuwa serikali imejipanga kikamilifu kuuendesha kwa mujibu wa sheria za uchaguzi.

Kuhusu mafuriko, alisema maeneo ya Rufuji na Morogoro yamekumbwa na mafuriko na kutoa pole kwa wananchi huku akiwaeleza kuwa wanawakumbuka katika maombi na kwamba wapo pamoja nao.

"Ahadi yetu kwenu tupo pamoja nanyi na tutahakikisha changamoto zote zinazotokea zinapatiwa ufumbuzi," aliahidi.

### MIAKA MITATU UONGOZI

Kuhusu miaka mitatu tangu aingie madarakani, Rais Samia alisema pongezi na dua zinampa nguvu na ari zaidi ya kutumikia watanzania na kuwaahidi kuendelea kuyafanya yale yatakayoleta ustawi na uimara kwao huku akiomba wadumishe amani na utulivu kwa kuwa, nia ya kufanya hayo wanayo.

"Ninashukuru kwa risala yenu mmegusia amani, maadili uchaguzi Serikali za Mitaa na utunzaji wa mazingira na msisitizo wa amani wa nchi yetu ambayo ni suala la msingi. Bila amani ibada haziwezi kufanyika," alisema.

Aidha, alionyesha kufurahishwa na jitihada zao za kupanda miti na kuwataka wahamasishe waumini waipande ikiwamo ya matunda, kivuli na ya mazao ya biashara ambayo yote ni sehemu ya hifadhi ya mazingira.

### SALAMU ZA BAKWATA

Katika Salamu za BAKWATA, Katibu Mkuu, Alhaj Nuhu Mruma, alisema: "Tunatambua hivi karibuni umetimiza miaka mitatu ya uongozi wako tukijivunia na falsafa yako ya R4 ambayo imeambatana na mambo makubwa yenye kuonekana katika sekta mbalimbali ikiwamo ujenzi wa madarasa, ujenzi wa reli, mtangamano wa siasa uliopanua wigo wa demokrasia na kukua kwa huduma za kijamii na kufungua uhusiano kimataifa.

Alhaj Mruma alisema wataendelea kumuunga mkono kwa kuwa, amedhihirisha uwezo mkubwa wa kuwa mama mlezi.

"Ulisisitiza kuangalia taasisi ya familia na kutoa takwimu zaidi ya nusu ya Watanzania wenye umri wa kuoa au kuolewa hawajaingia katika ndoa na mijini asilimia 61.5 na vijijini 5.5 waliofanikiwa kuingia katika ndoa kuna changamoto nyingi hasa ndoa changa na za vijana," alisema.

Mruma alisema kutokana na umuhimu wa familia, BAKWATA chini ya Ofisi ya Kadhi Mkuu wa Tanzania ilifanya utafiti kujua sababu za kuvunjika kwa ndoa ukihusisha mikoa sita hadi sasa.

Alisema matokeo ya awali yanaonyesha sababu ya migogoro na kuvunjika kwa ndoa ni mmomonyoko wa maadili asilimia tisa, kukosekana kwa uadilifu kwa asilimia nane na tatizo la afya ya akili asilimia saba.

Pia alisema kukosekana kwa elimu ya ndoa kwa asilimia 70 na sababu zingine ikiwamo matumizi mabaya ya simu, uasherati na kupungua kwa uvumilivu asilimia sita.

Aidha, alisema matokeo hayo yanaonesha kukosekana kwa elimu sahihi ya ndoa ndiyo sababu kubwa ya uvunjifu wa ndoa nyingi, hivyo ofisi hiyo imeandaa na mpango maalum itakayojumisha jamii, wafungishaji wa ndoa kwa kutumia mbinu na njia mbalimbali ili kunusuru taasisi hiyo ya ndoa. Pia alisema Mufti wa Tanzania, Shekhe Dk. Abubakari Zuberi bin Mbwana, ameandika kitabu maalum kinachohusiana na mmomonyoko wa maadili kinachojulikana kama 'Mmomonyoko wa Maadili Nani Alaumiwe' kitakachozinduliwa hivi karibu.

### UCHAGUZI

Mruma pia aligusia suala la uchaguzi ujao huku akibainisha kwamba ni jambo muhimu kwa mustakabali wa taifa na kuwahamasisha Watanzania kujitokeza kwa wingi katika kila hatua na wenye sifa wasiache kugombea kwa kuwa hiyo ni fursa ya msingi kikatiba.

BAKWATA kupitia kwa Alhaji Mruma, ilitoa wito kwa Waislamu na watanzania kuunga mkono juhudi za serikali na kutunza mazingira na kuwa na matumizi sahihi ya nishati mbadala.

Kuhusu Hijja baraza hilo limewataka waislam wajitahidi wasikose ibada hiyo kwa kuhakikisha wanajitokeza kwa wingi ili kutimiza nguzo hiyo hususan vijana, kwani idadi ya Watanzania ni ndogo ikilinganishwa na mataifa mengine wanaokwenda huko.

EID EL FITR

# Mbiu ya Katiba, uchaguzi yarindima Eid

**Na Waandishi Wetu**



Baadhi ya Waumini wa dini ya Kiislamu, wakishiriki swala ya Eid El Fitri katika Uwanja wa Jamhuri, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

MWANGWI wa Katiba mpya umejitokeza kwa viongozi mbalimbali kukumbusha huku Rais Samia Suluhu Hassan na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa wakihusia matendo mema wakati wote.

Jana, Rais Samia aliungana na waumini wenzake katika msikiti wa Mohamed VI, katika makao makuu ya Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA), Kinondoni, Dar es Salaam, kwa ajili ya swala ya Eid el-Fitr huku Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akiswali Unguja na Waziri Mkuu, Majaliwa katika Msikiti wa Ghadafi, Dodoma.

WARAKA WA EID

Katika sherehe hizo za Eid, Shura ya Maimamu Tanzania jana ilitoa waraka wa Idd, ukitaka dhamana ya uongozi wapewe wale waadilifu wenye utu na huruma kwa binadamu wenzao, wasipewe wasio na hisia za utu kwa wengine.

Pia waraka huo umegusia Katiba mpya na kuonyesha wasiwasi kwa yaliyotokea uchaguzi uliopita kujirudia katika uchaguzi ujao endapo suala hilo halitafanyiwa kazi.

Katibu Mkuu wa Shura ya Maimamu Tanzania, Shekhe Issa Ponda, akisoma waraka huo mkoani Dar es Salaam, alisema mwaka 2012 taifa lilianzisha mchakato wa kuandikwa Katiba mpya kwa lengo la kutatua matatizo, yakiwamo ya uongozi.

"Rasimu tarajiwa ilipatikana ikibeba maoni mengi ya wananchi. Matarajio yalikuwa Katiba Mpya italeta mfumo mpya wa uchaguzi wenye Tume Huru ya Uchaguzi. Pamoja na kila hatua muhimu kukamilika, mchakato huo ulizimwa, taifa likaingia tena katika uchaguzi mpya bila ya sheria zenye uwezo wa kutenda haki," alisema.

Kutokana na hilo, Ponda alisema wanaona uwezekano wa kutokea mabalaa kama yaliyokuwa katika chaguzi za nyuma ni mkubwa.

Shekhe wa Mkoa wa Iringa, Said Abri, aliwataka Watanzania kuendelea kudai katiba Mpya kwa amani pasipo vurugu.

Akitoa salamu za Eid baada ya ibada ya Eid iliyofanyika uwanja wa Samora mjini Iringa, Shekhe Abri alisema Rais Samia ameonyesha nia ya kutaka Katiba mpya na mara kadhaa amekuwa akisisitiza hilo.

"Suala la katiba mpya ni hitaji la Watanzania wote na si kikundi cha watu au mtu mmoja, hivyo itakuwa si busara kwa kikundi au mtu kufanya uchochezi au vurugu wakati wa kuhitaji katiba mpya," alisema.

Kuhusu Uchaguzi wa Serikali za Mitaa unaotarajiwa kufanyika mwaka huu na uchaguzi mkuu utakaofanyika mwakani Shekhe Abri alitaka watu wenye sifa ya kugombea kujitokeza kugombea nafasi hizo.

**MWINYI NA AMANI**

Katika salamu zake za Eid, Rais Dk. Mwinyi alisema kuwapo kwa amani na utulivu kuna umuhimu mkubwa wa kuwawezesha wananchi kutekeleza ibada zao kwa uhuru na usalama pamoja na kufanya shughuli za maendeleo.

Akitoa salamu hizo katika ibada iliyofanyika Ziwani Polisi mjini Unguja, alisema kwa kuzingatia kuwa kipindi cha sikukuu huwa na harakati nyingi zikiwamo za viwanja vya sikukuu na matumizi makubwa ya usafiri wa Barabara, ni muhimu Jeshi la polisi kwa kushirikiana na ofisi za mikoa na wilaya na vyombo vyote vya usalama kuimarisha ulinzi na usalama.

"Natumia fursa hii kuwaomba wananchi wenzangu tuendelee kudumisha amani kwa kila hali ili nchi yetu izidi kupiga hatua za maendeleo," alisema.

Pia aliwataka viongozi wa dini, mashekhe na walimu kuendelea kuiombea dua nchi na viongozi kuwa na amani na kwa pamoja Mwenyezi Mungu awezeshe kushirikiana katika kuzipatia ufumbuzi changamoto mbalimbali zinazoikabili nchi kiuchumi na kijamii.

"Tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kutujaalia uwezo wa kuitekeleza mipango yetu ya maendeleo, ikiwamo uimarishaji wa huduma za jamii za elimu, afya na maji katika baadhi ya maeneo. Jitihada za kukamilisha miradi mikubwa ya maji safi na salama nchini zikiwa katika hatua za mwisho," alisema.

Alisema ujenzi wa barabara mbalimbali unaendelea hasa katika manispaa ya mji wa Zanzibar, hivyo wananchi kuwa wastahamilivu kutokana na usumbufu wanaoupata unaosababishwa na shughuli za ujenzi wa barabara zinazoendelea.

Aidha, aliwashukuru waumini wa dini zingine kwa ushirikiano mkubwa walioutoa kwa ndugu zao waislamu katika kipindi chote cha Mwezi Mtukufu wa Ramadhani na kwamba hatua hiyo ni muhimu na kielelezo cha ustahamilivu na ustaarabu ambao nchi inaendeleza.

"Hali hii inapaswa kuendelezwa kwani ina mchango mkubwa wa kuifanya nchi yetu kuendelea kudumu katika amani, utulivu na umoja. Tunamuomba Mwenyezi Mungu atudumishe katika neema hii," alisema.

**WAZIRI MKUU**

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa aliwataka waumini wa dini ya Kiislamu kuendelea kuyaishi yale waliyojifunza wakati wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani ili kuhakikisha jamii inaendelea kuwa bora na kulifanya taifa kuwa lenye utulivu, amani na mshikamano.

Akizungumza kwa niaba ya Rais Samia kwenye swala ya Eid El Fitr iliyofanyika katika Msikiti wa Gadaffi jijini hapa, alisema kila mmoja anapaswa kufuata misingi iliyoimarishwa kwenye jamii ikiwamo kupinga na kukataa ukatili dhidi ya watoto, wanawake.

Alisema Rais Samia amekuwa mfano wa kuigwa katika kipindi cha Mwezi Mtukufu wa Ramadhani kwa kushiriki ibada ya futari na makundi mbalimbali katika jamii ambayo itawezesha kuijenga jamii yenye misingi imara. Majaliwa pia aliwataka Watanzania kuendelea kuliombea taifa ili liendelee kuwa na utulivu na amani.

Shekhe Mkoa wa Dodoma, Mustapha Rajabu, aliwashukuru viongozi wa serikali kwa kujitokeza kuwakumbuka watu wenye uhitaji kwenye kipindi chote cha mwezi Mtukufu wa Ramadhani.

Alisema kwa kushirikiana na viongozi wa dini wamewakumbuka watu wenye mahitaji katika kipindi cha Mwezi Mtukufu kama vile wafungwa na mahabusu, yatima, wajane wazee na kwenye vituo vya kulelea watoto.

"Kwa moyo huo kwa kweli sisi kama viongozi wa dini tuna kila sababu ya kuwashukuru kwa kuwakumbuka watu hao ambao mara nyingi wamekuwa wakisahaulika mara nyingi lakini kwa kushirikiana wamewapatia mahitaji mbalimbali," alisema.

**AMANI NA MSHIKAMANO**

Viongozi wa dini ya Kiislamu wamewataka wagombea katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa unaotarajiwa kufanyika mwaka huu, wametakiwa kulinda amani na mshikamano uliopo kwa kutambua kuwa katika uchaguzi, kuna kushinda na kushindwa, hivyo wasiwe sehemu ya kuhamasisha uvunjifu wa amani.

Akizungumza katika ibada ya Eid El Fitiri, Shekhe wa Wilaya ya Kahama, Alhaji Omary Damka, alisema mambo mengi yamekuwa yakiibuka katika uchaguzi, hivyo ni vyema kuhakikisha wanadumisha amani.

Shekhe Damka alisema wakati wa matokeo ya uchaguzi mkuu na wa Serikali za Mitaa, kumekuwa kukiibuka vurugu na kugomea matokeo yanayotangazwa na wasimamizi, hivyo kusababisha kuvunja amani.

Damka alisema kwa wale watakaoshindwa wakubali matokeo na kuungana na watakaoshinda kuleta maendeleo kwa wananchi.

Shekhe wa Mkoa wa Mwanza, Hassan Kabeke, akihutubia waumini katika swala ya Eid kwenye uwanja wa Nyamagana, aliwataka Waislamu kudumisha amani kuelekea kipindi cha uchaguzi sambamba na kushiriki kikamilifu katika shughuli zote za uchaguzi ikiwamo kujiandikisha katika daftari la kudumu la wapigakura.

Aliwataka kushiriki pia kuchukua fomu za kugombea nyadhifa mbalimbali kupitia vyama vya kisiasa kwa mujibu wa katiba ili wasije kuanza malalamiko baada ya uchaguzi kwamba viongozi hawafanyi vizuri ilihali hawakushiriki kuwaweka madarakani.

Pia alisema Sikukuu ya Eid inatoa fursa kwa familia kukutana na kujuliana hali sambamba na kuwasaidia maskini, yatima na watu wasiojiweza ikiwa ni mwendelezo wa kutenda mema kama ilivyokuwa wakati wa Mwezi Mtukufu.

Shekhe Kabeke pia alikemea matumizi ya dawa za kulevya ambazo zimekithiri kwa sasa hususani matumizi ya mirungi ambayo alisema yameharibu idadi kubwa ya vijana.

**Romana Mallya (DAR), Rahma Suleiman (ZANZIBAR), Peter Mkwavila, DODOMA, Fransis Godwin, IRINGA, Vitus Audax na Shaban Njia, KAHAMA.**




Mwenyekiti wa kampeni ya kuwawezesha wanawake kushinda uchaguzi wa Serikali za Mitaa ya "Mwezeshe ashinde", Mary Mushumbusi akizungumza katika mkutano wa kuzindua kampeni hiyo, katika Kata ya Kipunguni, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Mafuriko yaua, timu ya wataalamu, mawaziri yapelekwa Rufiji

**Gwamaka Alipipi na Halfani Chusi**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa amesema timu ya mawaziri itakwenda Rufiji na Kibiti, mkoani Pwani kuungana na timu ya wataalamu kufanya tathmini ya pamoja ya athari zilizosababishwa na mafuriko yaliyokumba wilaya hizo.

Kukiwa na hatua hiyo serikalini, watu wawili wameripotiwa kufariki dunia wakati wanajiokoa kwa kutumia mtumbwi. Imeelezwa kuwa wawili hao; mama wa miaka 35 na mtoto wa mwaka mmoja, walifariki dunia baada ya mtumbwi wao kugongwa na gogo na kupoteza mwelekeo.

Majaliwa alitoa taarifa hiyo juzi jijini Dodoma wakati wa hafla ya futari aliyoiandaa kwa ajili ya watumishi wa ofisi yake na taasisi zilizo chini ya ofisi hiyo.

"Sisi ndiyo tunaratibu idara ya maafa kitaifa. Hapa tunapozungumza, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), Jenista Mhagama pamoja na Katibu Mkuu, Dk. Jim Yonaz wako njiani wanaelekea mkoani Pwani.

"Mto Rufiji umejaa na kata nne zimo kwenye maji, mawaziri wengine wa kisekta ikiwamo afya, kilimo, mifugo nao pia wanakwenda ili kuimarisha uratibu wa zoezi," alisema.

Hadi sasa mafuriko wilayani Rufiji yamesababisha athari mbalimbali, ikiwamo kaya zaidi ya 2,500 katika Kata ya Muhoro kukosa makazi, zaidi ya wananchi 10,000 wilayani humo wakiathirika.

Wiki iliyopita, Waziri Mkuu Kivuli wa Chama cha ACT Wazalendo, Isihaka Mchinjita, alimtaka Waziri Mkuu kufika Rufiji na Kibiti kuona hali halisi na kuhakikisha hatua stahiki za kunusuru wananchi zinachukuliwa.

Juzi, Makamu Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Abdulrahman Kinana, alitaka serikali kuharakisha huduma kwa wananchi wa Rufiji waliopata mafuriko.

**VIFO WATU WAWILI**

Mkuu wa Wilaya ya Rufiji, Meja Edward Ndowelle, aliiambia Nipashe jana kuwa serikali ilitoa maelekezo watu wasitumie mitumbwi, lakini baadhi waliamua kutumia kama njia ya kujiokoa.

"Mtumbwi ulikuwa na watu watano, baada ya gogo kuugonga, watatu walijiokoa na wawili walishindwa kujitokoa na kupoteza maisha. Hadi sasa hakuna vifo vingine," alisema.

Meja Ndowelle alisema mwaka huu kumekuwa na vifo vichache kutokana na mafuriko katika eneo hilo kulinganishwa na miaka ya 1978 na 1998.

Alisema Bwawa la Nyerere lilipoanza kujaa, dalili zilionekana si njema na wananchi waliekezwa kuchukua tahadhari ikiwamo kuwahamisha waliokuwa kwenye maeneo hatarishi.

Kwa mujibu wa Ndowelle, kuna kikosi kazi cha uokoaji kimepiga kambi eneo hilo kwa ajili kuhamisha waliozingirwa na maji.

"Wanatumia boti mbalimbali kutoka Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA) na Wakala wa Misitu Tanzania (TFS). Hivyo, hali inazidi kuimarika kwa kuwa wananchi wengi wanazidi kuokolewa wakati maji yakiongezeka," alisema.

Mkuu wa Wilaya pia alisema serikali imetenga eneo katika Kata ya Muhoro kwa ajili ya kugawia viwanja waathirika wa mafuriko hayo.

"Tunashukuru misaada imeanza kumiminika ikiwamo shehena ya vyakula imeanza kumininika kutoka serikalini na sekta binafsi, mahitaji ni mengi, tunawaomba Watanzania kokote waliko wawasaidie wenzao," alisema.

Wakizungumza na Nipashe, baadhi ya wananchi, akiwamo mama lishe katika Kijiji cha Muhoro, Halima Mwenzegule, walisema amepata hasara kwa kuwa mali zao zote zimezolewa na mafuriko. Sasa hawana mitaji na hawajui pa kuanzia.

Mkazi wa Kijiji cha Muhoro, Bakari Seif, aliomba serikali kuwapa fidia wafanyabiashara waliopoteza mali zao kwa kuwapatia mitaji ili warudi kwenye shughuli zao.

Katika Iftari ya juzi, Waziri Mkuu Majaliwa pia alipongeza Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA) namna inavyodhibiti biashara ya dawa za kulevya nchini.

"Kamishna amefanya kazi nzuri na kuboresha kwenye sekta yake, hivi sasa taasisi yake haishii tu makao makuu ya nchi, ameshusha kwenye kanda na tayari wakurugenzi wameshakwenda kwenye maeneo hayo ambao watakamata wazalishaji, wasafirishaji, wafanyabiashara na watumiaji dawa za kulevya," alisema. Viongozi wengine walioshiriki katika Iftari hiyo ni Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Deogratius Ndejembi na Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), Ummy Nderiananga.

Wengine ni Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Mary Maganga na wakuu wa taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

# Tisa wafariki dunia, 19 wajeruhiwa ajali ya basi

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

WATU tisa wamefariki dunia na wengine 19 kujeruhiwa baada ya basi la Kampuni ya Lujiga Express lililokuwa linatoka Dar es Salaam kwenda Mwanza, kugonga lori la mizigo kwa nyuma kijijini Malendi, Kata ya Mgongo, wilayani Iramba.

Mkuu wa Wilaya ya Iramba, mkoani Singida, Suleiman Mwenda, aliiambia Nipashe jana kuwa ajali hiyo ilitokea juzi saa 10:30 alfajiri katika kijiji hicho, akifafanua kuwa lori lililogongwa na basi hilo lilikuwa limeegeshwa barabarani kutokana na kuharibika.

Alisema ajali hiyo imehusisha basi la Kampuni ya Lujiga Express lenye namba za usajili T 315 CXX ambalo lilikuwa linatoka Dar es Salaam kwenda Mwanza.

Alisema kuwa kati ya waliofariki dunia, wanaume ni sita; maiti zimehifadhiwa katika Hospitali ya Wilaya ya Igunga, mkoani Tabora.

Suleiman alisema majeruhi wa ajali hiyo wamelazwa katika Hospitali ya Wilaya ya Iramba (Kiomboi) na wengine katika Hospitali ya Wilaya ya Igunga ambako wanaendelea na matibabu.

Mkuu wa Wilaya alisema basi hilo lilipofika katika Kijiji cha Malendi, kulikuwa na lori la mizigo ambalo lilikuwa limeegeshwa pembeni ambalo nalo lilikuwa limetoka Dar es Salaam likielekea Mwanza; liligongwa na kusababisha vifo na majeruhi hao.

Mkuu wa Wilaya hakutaja majina ya waliofariki dunia wala majeruhi, akiahidi kuwa taarifa zaidi za tukio hilo zitatolewa na Jeshi la Polisi.

# Ujenzi wa vyoo waanza shule wanakojisaidia vichakani

**Na Waandishi Wetu,** SONGEA

SIKU chache baada ya gazeti hili kuripoti kuhusu hatari inayokabili wanafunzi na walimu wa Shule ya Msingi Tembo Mashujaa, mjini Songea, mkoani Ruvuma, wanaojisaidia vichakani kwa miaka mitatu kutokana na vyoo kujaa, hatimaye ujenzi wa matundu manne ya vyoo shuleni huko umeanza.

Waandishi wa gazeti hili wameshuhudia mafundi wakichimba shimo la choo pembezoni mwa choo cha awali.

Mwenyekiti wa Kamati ya shule hiyo, Masumbuko Mbogoro, aliiambia Nipashe jana kuwa baada ya taarifa hiyo kuchapishwa gazetini, hatua zimeanza kuchukuliwa na Manispaa ya Songea.

Alisema kuwa manispaa kupitia Kata ya Bombambili, imeanza kuchimba shimo la choo na msingi kwa ajili ya jengo la choo, akibainisha kuwa wanajenga choo chenye matundu manne na mkandarasi yuko eneo la ujenzi.

Hata hivyo, shule hiyo yenye zaidi ya wanafunzi 800, inahitaji kujengwa choo chenye matundu 32 ili kukidhi uwiano unaokubalika kisera wa 1:25; yaani wavulana 25 kwa tundu la choo au 1:20 (wasichana 20 kwa tundu).

Mwalimu Mkuu wa Shule hiyo, Mary Mpyambala, pia alithibitisha kuanza kwa ujenzi huo, akisema: "Sh. milioni tano kwa ajili ya ujenzi huu ni ndogo. Na matundu manne bado ni machache kwa wanafunzi wapatao 800. Matundu ya zamani hayawezi kutumika tena, yanatitia.

"Fedha hiyo ni kidogo, hivyo walimu nao hawana namna, inabidi watumie matundu hayo hayo manne, yanayoendelea kujengwa kwa ajili ya wanafunzi, tunawaomba Watanzania watusaidie katika hili."

Jumapili iliyopita, waandishi wa Nipashe walifika shuleni huko, umbali wa Km 3.8 kutoka mjini Songea na kubaini choo kimejaa. Kwa mujibu wa Mwalimu Mkuu Mary, walimu 17 wa shule hiyo yenye zaidi ya wanafunzi 800 hawana vyoo, walikuwa wanatumia matundu 10 ya choo cha wanafunzi wao ambacho kilishajaa miaka mitatu iliyopita, hivyo wanafunzi na walimu hao kujisaidia vichakani.

***Imeandaliwa na Christina Mwakangale na Gideon Mwakanosya**

# EID EL FITRI KATIKA PICHA



Rais Samia Suluhu Hassan akisalimiana na Shekhe Mkuu wa Tanzania Mufti Abubakar Zuberi kabla ya kuanza kwa ibada ya Eid El Fitri katika Msikiti Mkuu wa Mfalme Mohammed VI wa Morocco, Kinondoni Dar es Salaaam, jana. **PICHA: IKULU**



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akizungumza na waumini wa dini ya kiislamu kwenye Sala ya Eid El Fitri katika Msikiti wa Gaddafi, jijini Dodoma jana. **PICHA: OWM**



Mwenyekiti wa Bodi ya Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi nchini, Balozi Adadi Rajabu (katikati), akijadiliana jambo na Mkurugenzi wa TSN, Faroughu Baghoza (kulia) na Mzee Juma Nyongo, baada ya kumalizika kwa sala ya Eld El-Fitri katika msikiti mkuu wa Ijumaa wilayani Muheza, mkoani Tanga jana. **PICHA: STEVEN WILLIAM**



Baadhi ya wananchi wakichagua kuku katika soko la Mwananyamala, jijini Dar es Salaam jana, kwa ajili ya kujipatia kitoweo katika Sikukuu ya Eid El-Fitri. **PICHA: MIRAJI MSALA**



Waziri wa Madini na Mbunge wa Jimbo la Dodoma, Anthony Mavunde (wa tatu kushoto), akikabidhi msaada wa vyakula kwa Mwenyekiti wa Chama Cha Albino Mkoa wa Dodoma, Julius Ludovick vilivyotolewa kwa ajili ya vituo vya watoto yatima pamoja na wajane kwa ajili ya mfungo wa Ramadhani uliohitimishwa jana. Katikati ni Shekhe wa msikiti wa Gadafi, Mustapha Rajabu. **PICHA: PETER MKWAVILA**



Akinamama waliojumuika kwenye sala ya Eid El Fitri, wakifuatilia ibada katika Msikiti wa Gadafi, jijini Dodoma jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mabilioni yaliyotengwa kuwakopesha wajasiriamali yalete matokeo chanya

**WAJASIRIAMALI** wadogo nchini wametangaziwa neema kutokana na Benki ya Biashara Tanzania (TCB) kutenga Sh. bilioni 300 kwa ajili ya kuwakopesha ili kupanua wigo wa ajira na kuchochea kasi ya ukuaji wa uchumi kwa mwaka 2024.

Hatua hiyo ni ya kupongezwa na ya kupigiwa mfano kwa sababu kwa idadi ya walengwa 2,000 katika mpango huo ni dhahiri kwamba kutakuwa na matokeo chanya katika biashara. Kuwawezesha wafanyabiashara wadogo ndio msingi mkuu wa ukuaji wa biashara na uchumi katika taifa lolote ndiyo maana kuna msemo kwa hata mbuyu ulianza kama mchicha.

Msemo huo unasadifu na mpango huo wa TCB katika kukuza uchumi wa nchi kwa sababu mara nyingi watu wamekuwa wakilalamika kuwa kikwazo cha kufanya biashara kwao ni ukosefu wa mitaji, sasa fursa imepatikana kwa hiyo wale wanaokidhi vigezo na masharti hawana budi kukichangamkia.

Kama alivyosema Ofisa Mtendaji Mkuu wa TCB, Adam Muhayo, wajasiriamali wadogo wanachangia asilimia 30 katika ukuaji wa uchumi, ni wazi kwamba kuwapo kwa fursa hiyo kutasaidia kwa kiasi kikubwa kukua kwa Uchumi katika ngazi za familia kwa kuwa wajasiriamali hao watajiongezea kipato na kujikwamua kiuchumi. Kwa maneno mengine, umaskini wa hali na wa kipato utapungua miongoni mwa Watanzania kupitia wajasiriamali hao.

Hakika TCB imeona mbali kwa kuwawezesha wajasiriamali hao kwani ndio mpango mzima katika maendeleo ya biashara kutoka wajasiriamali wadogo, wa kati na wakubwa ambao mwisho huwa wafanyabiashara wakubwa na maarufu ambao pia ni tegemeo kubwa katika ulipaji kodi na ukuaji wa uchumi kwa ujumla.

Katika historia ya wafanyabiashara duniani kote, hakuna aliyezaliwa akiwa milionea au bilionea bali wote walianza katika hatua za chini huku wakikuza mitaji yao na kupanua biashara kulingana na fursa zilizokuwa na zinazoendelea kujitokeza.

Kwa mantiki hiyo, kutafungua fursa nyingi za kibiashara hasa uzalishaji na kuongeza thamani kama lengo la uwezeshaji huo. Pia kuwezeshwa kwa wajasiriamali hao kutasaidia kuongeza ajira miongoni mwa Watanzania kwa kuwa biashara zao zinapokua, watakuwa na uwezo wa kuajiri watu kusaidia shughuli na ukuaji wake na pia ongezeko la bidhaa na mzunguko wa fedha.

Pamoja na ukweli huo, ni wakati sasa kwa wajasiriamali wadogo kuchangamkia fursa hiyo na kutekeleza kwa vitendo katika uzalishaji mali na hatimaye kupanua mitaji na wigo wa biashara kwa ujumla. Hiyo inatokana na ukweli kwamba kilio chao kuhusu mitaji kimesikika baada ya benki hiyo kutangaza kuwa imetenga mabilioni hayo.


Suala lingine ambalo wajasiriamali hao wanapaswa kuzingatia ni uaminifu katika matumizi ya fedha hizo kwa lengo lililokusudiwa kwa kufanya biashara badala ya kuchepusha na kufanya mambo mengine kama sherehe, kununua nguo na samani na hata kuoa wake wa nyongeza.

Wajasiriamali hao pia wanapaswa kuwa waaminifu kama urejeshaji wa fedha hizo kwa sababu hazijatolewa kama hisani wala msaada bali mikopo, hivyo wanatakiwa kuheshimu mikataba ya upatikanaji wake.

Kwa muda mrefu, uzoefu unaonyesha kwamba baadhi ya watu wanapopata mikopo kutoka taasisi za fedha, hawazitumii kwa malengo yaliyokusudiwa bali huzielekeza kwenye sherehe, ndoa na kununua vitu kwa ajili ya matumizi ya nyumbani. Pia baadhi ya wakopaji wamekuwa hawarejeshi mikopo kama mikataba inavyoelekeza hadi wakopeshaji kuchukua hatua za kuwatangaza kupitia vyombo vya habari, kupokwa mali na kupigwa mnada.

Ni vyema wahusika wa mabilioni hayo yaliyotengwa na TCB yakatumika na wajasiriamali kwa malengo kusudiwa ili kuwawezesha kukuza biashara na kujikwamua kiuchumi na hatimaye kuchangia ukuaji wa Uchumi kwa ujumla.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Tutafakari kwa kina, taka zinazidi zama hizi za mvua

Na Joyce Lameck

**MAENEO** mengi jijini Dar es Salaam, yamezungukwa na taka. Hiyo ni kwa sababu ya kukosekana utaratibu mzuri wa kuzikusanya na kupelekwa katika madampo, magonjwa ya mlipuko yanatokea kwa sababu uchafu, kwani mvua sasa zimeshaanza.

Kimsingi, kuwapo kwa mazingira machafu ni hatari kwa afya, kwani ni chanzo cha magonjwa ya mlipuko katika jamii, maeneo mengi huonekana na taka zimejaa kwa muda mrefu, hadi kuzalisha wadudu wanaoweza kusababisha magonjwa hayo.

Magonjwa ya mlipuko yanatajwa kushamiri katika msimu wa masika kama unaoendelea sasa. Nionavyo ni kwamba, hiyo inatoa msukumo mkubwa wa kijamii katika kutaka kubadilishwe utaratibu wa kukusanya taka kwa wakati, ili kuepuka maradhi kama vile kipindupindu.

Ndani ya mtazamo huo, ndio nami natoa mchango wa mawazo ya awali kwamba kila mwenye nafasi ya kusukuma mabadiliko stahiki.

Mbali na kuwapo kwa magari ya kubeba uchafu, bado kuna maeneo mengi tu ambayo hayafikiwi na magari hayo na kuchangia uchafuzi wa mazingira, kwani taka zinatupwa ovyo kila mahali, katika mazingira ambayo nayo si ya busara hata kidogo.

Hata maeneo ambayo yana huduma ya magari yanayobeba taka na kupeleka kwenye madampo, bado ni changamoto kwani hayafiki kwa wakati, hata kusababisha kulundikana uchafu mara nyingi, ikiwekwa pembezoni mwa barabara.

Serikali inapaswa kuangalia suala hili kwa jicho la tatu, ili kuweza kukomesha tatizo hili la mlundikano wa taka katika maeneo mbalimbali kabla ya magonjwa kushambulia watu.

Ihakikishe magari yanafika kenye maeneo yote katika mkoa mzima, ili ziwekwe sheria ambazo zitawafanya wananchi waweke mazingira safi kwa kuzihifadhi vizuri, kabla ya kuchukuliwa na magari ya kubeba taka na kuzisafirisha kwenye madampo makubwa.

Kwa mtazamo wangu jamii inapaswa kuwekewa sheria ambazo zitasaidia kuweka mazingira safi na kuepuka maradhi yatokanayo na mlundikano wa taka kwenye maeneo yanayotuzunguka.

Jamii kwa pamoja tukishirikiana na serikali, tunaweza kuweka mazingira safi na kufanya afya zetu ziwe imara na kuendelea kufanya kazi kwa ajili ya kukuza uchumi wa taifa letu, kizazi cha sasa na kijacho.

Kama zilivyo tafsiri za busara nyinginezo, mara zote tunapotafakari haya huwa napenda tusiingie katika kumbukumbu zetu kihistoria na kimaisha, kwamba dhana mazingira ilivyochukua nafasi, hata kiutawala maisha yetu katika mabadiliko hayo mapya.

Ndiyo maana hata kijamii, ndani ya nguzo zetu za kiserikali, mahitaji hayo ya kimazingira yanachukua uso wa kisekta zikipatiwa wizara, huku nchini Mazingira ikiwa chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira, ikithibitisha mazingira inabaki kuwa 'kila kitu'.

Ni jambo linaloenda mbali ni kwamba kadri mtu anapojali dhana hiyo ya mazingira, inaenda mbali kwa kujikuta anagusa mambo mengi kuanzia tafsiri ya maisha ya mtu mmoja mmoja, hadi kwa makundi.

Kupitia huo usemi 'inawezekana, timiza wajibu wako' kila mmoja wetu, hadi nguzo ya juu serikalini, nikimaanisha wizarani na ngazi zinazofanana nazo.

Mathalan, maamuzi makuu ya ngazi za huko juu, katika mustakabali huo wa mazingira, haishangazi ikamgusa kila mmoja wetu.

Ndicho ambacho hata tukishuka nacho mahali tuliko, katika maisha yetu yaliko tukiwa mabalozi wa vitendo katika stadi ya mazingira tukikabili kuona kadri yanavyotakiwa kwenda.

Hilo jambo bado ni bora zaidi, kwamba inapaswa tukasaidiana katika mahali tuliko katika kuboresha mwenendo wa kutetea usafi na ufanisi katika mazingira tunayoishi kuleteana maendeleo ya kimaisha.

Inapendeza sana, hata kila mmoja wetu akafikia maisha ni utamaduni wake, kama alivyo muumini wa kidini, naye akawa muumini wa kimazingira, hata akawa anayapigania zaidi katika mustakabali wa kiimani na kiutamaduni, zaidi ya kuifanya kisheria, kila la kheri tutakiane, naamini inawezekana, daima isishindikane.

## HABARI KITAIFA

# Ukuta wa uzio wa jirani waanguka ukiua watu wawili wa familia moja

**Na Godfrey Mushi,** ARUMERU

WATU wawili wa familia moja wakazi wa Kijiji cha Ilkirevi, Kata ya Olturoto, Wilaya ya Arumeru, mkoani Arusha, wamepoteza maisha baada ya nyumba waliyokuwa wamelala usiku wa manane kuangukiwa na uzio wa jirani yao.

Waliopoteza maisha ni baba mzazi wa familia hiyo, Loriv Noah na mwanawe Glory Noah, huku mama wa mtoto huyo (jina lake halijatajwa) akinusurika baada ya kuangukiwa na ukuta.

Akizungumzia tukio hilo jana, kaka wa marehemu, Abraham Noah, alisema wakati tukio hilo linatokea, ndani ya nyumba hiyo kulikuwa na watu wanne; baba, mama na watoto wawili.

"Kweli ni jambo la kusikitisha sana kwa sababu ya mvua nkubwa iliyonyesha usiku wa Aprili 8, 2024, ndio zimesababisha vifo hivi. Hili tukio lilitokea saa sita na dakika kadhaa usiku.

"Nikiwa nimelala tayari, kuna kijana alikuwa analala na wazazi wake kwenye nyumba iliyoangukiwa na ukuta (amenusurika), aliniamsha akiniambia baba njoo, wazazi wangu wameangukiwa na ukuta.

"Niliamka haraka na kukimbia nikawa wa kwanza kufika pale, mimi na shemeji yangu tukapiga kelele watu wakatoka kutusaidia. Mke wa marehemu tulikuta ukuta wa nyumba ulioangukiwa na uzio, umemfunika kuanzia miguuni mpaka kifuani.

"Tukajitahidi tukamwondoa na kumkimbiza hospitalini. Tukajitahidi kumwokoa mumewe (Loriv), lakini tukakuta tayari ameshaaga dunia na mtoto wake pia vivyo hivyo (Glory). Baba na mtoto wao waliangukiwa na ukuta wote wa nyumba baada ya kulaliwa na huo uzio," alisimulia.

Kwa mujibu wa kaka huyo wa marehemu, uzio ulioanguka kutokana na mvua hizo, uliangukia nyumba ya ndugu yake iliyokuwa imejengwa bondeni- pembezoni mwa uzio huo. Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Ilkirevu, Abraham Mollel, alisema kutokana na tukio hilo la kupoteza watu wawili wa familia moja, watapita kila nyumba kukata miti yote mikubwa iliyoko pembezoni mwa nyumba ili kuepusha madhara ya miti kuangukia nyumba na kuacha maafa. Mbunge wa Arumeru Magharibi (CCM), Noah Lembrice, akizungumza jana na wakazi wa Ngaramtoni, wilayani humo alitoa pole kwa familia zote zilizopoteza wapendwa wao na wale waliopoteza makazi kutokana na mafuriko ya mvua inayoendelea kunyesha.

Mbali na watu hao wa familia moja kupoteza maisha, mbunge huyo alisema pia amepokea taarifa nyingine ya watu wawili waliosombwa na mafuriko.

"Nina taarifa mpaka sasa tumepoteza watu wawili kwa kusombwa na mafuruko kutokana na mvua inayoendelea kunyesha. Mtu mmoja kutoka ukanda wa Ngaramtoni na mtu mmoja ukanda wa Ilkiding'a," alisema.

Akiwa Kijiji cha Ngaramtoni alikokwenda kutoa pole na kuzungumza na wananchi, mbunge huyo alitaka wananchi wa jimbo hilo kuchukua tahadhari kutokana na mvua inayoendelea kunyesha. Katika mkutano huo, Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Olevolosi kilichoko kata ya Kimnyak, Emanuel Ngailuva, alimweleza mbunge huyo kuwa wamepata changamoto ya kumpoteza kijana wao baada ya kusombwa na mafuriko katika Mto Seliani, ambao umefurika na hauna kivuko.



Mabalozi wa Shirika la Akili Platform Tanzania (APT), wakifanya usafi eneo la ufukwe wa Coco, jijini Dar es Salaam jana, ikiwa ni sehemu ya mchango wao katika kutunza mazingira. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Wasichana 10,000 warejea shuleni baada ya kukatisha masomo yao

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

WASICHANA 10,239 waliokatiza masomo ya elimu ya sekondari kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo kupata ujauzito, wamesajiliwa kupata fursa ya kuendelea na masomo hayo kwa njia mbadala katika mikoa ya Tanzania Bara kwa kipindi cha miaka mitatu ya masomo kuanzia 2012/22 hadi 2023/24.

Wasichana hao waliokatisha masomo wamepata fursa hiyo kwenye Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima Tanzania (TEWW) kupitia utekelezaji Mradi wa Uboreshaji Elimu ya Sekondari kwa Njia Mbadala (SEQUIP – AEP) unaotekelezwa Tanzania Bara.

Kaimu Mratibu wa mradi huo, Amina Abubakar alisema hayo mjini Morogoro wakati wa mafunzo ya waratibu wa vituo wa mikoa 26 ya Tanzania Bara yaliyolenga kuwajengea uwezo katika kuboresha usimamizi na uendeshaji elimu na mafunzo ya elimu ya sekondari kwa njia mbadala.

Alisema wasichana hao ni walikatiza masomo ya elimu ya sekondari kwa sababu mbalimbali ikiwamo kupata ujauzito ambao ni wenye umri kati ya miaka 13 hadi 21 na kupata tena fursa ya kuendelea na masomo ya sekondari kwa njia mbadala.

Alisema serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia pamoja na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kwa kushirikiana na Benki ya Dunia (WB), inatekeleza mradi huo wa miaka mitano kuanzia 2021 hadi 2026 wa maboresho ya elimu nchini.

Kaimu Mratibu wa Mradi huo alisema taasisi hiyo imepewa jukumu la kuimarisha utolewaji programu ya elimu ya sekondari kwa njia mbadala ijulikanayo kama SEQUIP – AEP kwa wasichana waliokatiza masomo ya elimu ya sekondari kwa sababu mbalimbali.

Amina alisema malengo mahususi ni kuongeza ufikiwaji wasichana walioshindwa kuendelea na elimu ya sekondari kwa sababu mbalimbali ikiwamo ugonjwa, hadi duni ya maisha au kupata ujauzito.

Kaimu Mratibu wa mradi huyo alisema mradi huo umelenga kuwafikia wasichana wapatao 12,000 nchini kote katika kipindi hicho cha miaka mitano.

Amina alisema mradi huo ulioanzishwa na serikali kwa sasa umeleta mafanikio kwa wasichana waliokatiza elimu ya sekondari ya mfumo rasmi na kupata fursa ya kujiunga kuendelea na masomo ya sekondari kwa njia ya elimu mbadala chini ya mradi huo.

Alisema taasisi imepewa lengo la kila mwaka kusajili wasichana 3,000, lakini kutokana na mwamko uliojitokeza kwa walengwa, idadi ya wanaosajiliwa imekuwa ikivuka lengo kila mwaka.

Amina alisema kwa mwaka wa kwanza wa masomo 2021/22 wasichana 3,333 walisajiliwa, mwaka 2022/23 wasichana 3,616 na mwaka 2023/24 wasichana 3,299 walisajiliwa kabla ya kufikia mwisho wa usajili wa masomo Machi 30, 2024.

"Tumepewa malengo kila mwaka tusajili wanafunzi 3,000 lakini uzuri kila mwaka tunavuka lengo tulilopewa na katika kipindi cha miaka mitano tunatakiwa tusajili wanafunzi 12,000 na huu ni mwaka watatu tayari tumesajili wasichana zaidi ya 10,000 " alisema Amina.

Aliongeza kuwa wanafunzi waliosoma mwaka jana (2023) katika hatua ya kwanza na waliofanya Mtihani wa Maarifa wa Taifa (QT) waliofaulli walikuwa ni asilimia 44 na wa hatua ya pili walifanya Mtihani wa Taifa wa Kidato cha Nne, waliofaulu walikuwa ni asilimia 68.

Alisema kuwa mbali na kuwapo mafanikio hayo, pia zipo changamoto kadhaa wanazokutana zao waratibu wa vituo mikoani kwenye utekelezaji mradi ambazo ni pamoja na utoro rejareja wa wanafunzi kufika kwenye vituo vya kusomea.

Alitaja utoro huo wa rejareja wa wanafunzi unachangiwa na baadhi yao wanatoka maeneo ya mbali kuvifikia vituo wanakosomea na wengine wana watoto tayari na wanakosa walezi wa kuwaachia.

Kaimu Mratibu wa Mradi huo alisema baadhi ya wasichana hao wamekuwa na changamoto zinazohusiana na familia, hali duni ya kifamilia (kipato) na wengine kufeli mtihani (mdondoko) kunakochangiwa na umbali wanakotoka.


Alisema katika kukabiliana na changamoto hizo, baadhi ya wadau wenye hosteli karibu na vituo, wamejitolea kuwachukua na kuishi kwenye hosteli hizo.

Alisema taasisi pia inatumia hosteli za Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi ili kupunguza mdondoko ama utoro rejareja ambao unajitokeza kwenye vituo.

Mratibu wa Taasisi hiyo Kituo cha Sabasaba, mkoani Mtwara, Fatuma Juma alisema kuanzisha mradi huo kumeweza kuwapa fursa wasichana ambao walikatiza masomo yao kutokana na sababu mbalimbali fursa ya kurudia masomo yao ya sekondari kwa njia mbadala.

## KABWELA

**Na Fadhili Mohammed**





Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akitoa mchango kwa ajili ya maandalizi ya futari kutoka kwa NMB kwa watoto wanaolelewa katika kituo cha kulea watoto wanaoishi katika mazingira magumu cha Umrah Orphanage wakati wa hafla ya futari iliyoandaliwa na benki hiyo jijini Dar es Salaam hivi karibuni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# 'Ramadhan 2024 ilikuwa ya kipekee kwetu'

## -Vituo saba vyenye watoto zaidi ya 1,000 vyapewa misaada. Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar, Spika, PM waipongeza...

**Na Mwandishi Wetu**

KUFUTURISHA wateja wake walio kwenye Mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhan, umekuwa ni utamaduni endelevu kwa Benki ya NMB.

Kila mwaka katika kila kipindi cha utekelezaji ibada ya funga ambayo ni Nguzo ya Pili kati ya tano za Kiislamu, NMB kupitia Programu ya Uwekezaji kwa Jamii (CSI - zamani CSR), hukutanisha pamoja wateja wake pamoja na wadau wengine wakiwamo viongozi wa serikali.

Ni kupitia hafla hizo za Iftar, NMB huwaweka pamoja wateja wao kutafakari maadili yanayounganisha binadamu wote, upendo kwa familia zao, shukrani kwa Mwenyezi Mungu, lakini pia toba na kuzidisha ushirikiano katika ibada.

Katika hafla ya kwanza, mjini Unguja, mwaka huu, Ofisa Mtendaji Mkuu wa NMB, Ruth Zaipuna alisema: "Umekuwa ni utamaduni endelevu wa NMB kuandaa futari katika kipindi hiki cha Ramadhani na mara zote tumekuwa tukialika wateja wetu, wadau na wageni wengine katika futari hizi.

"Pamoja na kuwaalika wateja wetu, viongozi na wadau mbalimbali, NMB imetumia fursa hii kujumuika na watoto kutoka katika vituo vya yatima na wanaoishi kwenye mazingira magumu, ambao wameungana nasi na watapokea misaada mbalimbali.

"Sisi NMB tunaamini kuwa kuwapo watoto hawa ni fursa ya wao kujifunza na kuendelea kuhamasika katika kutenda mema na kuwa wakarimu kwa jamii inayowazunguka.

"Tunawasihi watoto hawa waendelee kukua katika imani, wamtegemee Mwenyezi Mungu na wazidishe juhudi maishani, Mungu atawasaidia," alisema Bi. Zaipuna.

**MISAADA KWA WAHITAJI**

Kwa mujibu wa Zaipuna, katika Ramadhan ya mwaka huu, utaratibu huo uliongezwa thamani na NMB, ambako ilizitumia hafla hizo kuwaalika watoto yatima na wanaoishi kwenye mazingira magumu, kufuturu nao pamoja, kisha kuwapa misaada mbalimbali ya kijamii kwa ajili ya mwendelezo wa funga zao na sikukuu ya Eid el Fitr.

Zaidi ya watoto 500 walihudhuria hafla mbalimbali za NMB Iftar zilizofanyika Unguja, Pemba, Dar es Salaam na Dodoma, huku misaada waliyopewa ikienda kugusa zaidi ya watoto 1,000 walio kwenye vituo saba vilivyonufaika na bidhaa za mamilioni ya shilingi walizopewa na NMB.

Mjini Unguja, Makamu wa Pili wa Rais wa SMZ, Hemed Suleiman Abdulla, alipokea misaada hiyo kutoka kwa Ofisa Mtendaji Mkuu wa NMB, Zaipuna, kisha naye kuikabidhi kwa viongozi na walezi wa vituo vya Kidundo Orphanage Center na Mazizini Orphanage Center vya Zanzibar.

Ilikuwa hivyo pia jijini Dar es Salaam, ambako Waziri Mkuu wa Tanzania, Kassim Majaliwa, alipokea misaada mbalimbali ya kijamii kutoka kwa ofisa Mkuu wa Fedha, Juma Kimori, kabla ya Mtendaji Mkuu huyo wa Shughuli za Serikali Bungeni kuikabidhi kwa wenye uhitaji kutoka Tanzania Kwanza Orphanage, Al Zam Orphanage Center na Umrah Orphanage Center.

Spika wa Bunge la Tanzania, Dk. Tulia Ackson, naye akaingia katika orodha ya viongozi wakuu wa serikali waliopokea misaada ya NMB, wakati wa Iftar bungeni, kisha naye kuikabidhi kwa viongozi wa watoto wanaolelewa na Zamzam Islamic na Darul Maarifa, vituo vilivyo chini ya Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA) - Jiji la Dodoma.

"Kwa hili NMB mmefanya jambo kubwa sana, mnataka watoto hawa wajione kuwa wana thamani sawa na wengine. Kama ambavyo nimetoa wito kwa taasisi na wadau wengine kuiga kwa NMB. Nitumie fursa hii pia kuziagiza Mamlaka za Serikali za Mitaa - ambazo ni taasisi ya serikali, lichukueni hili kama ajenda," alisisitiza Waziri Mkuu Majaliwa na kuongeza:

"Hakikisheni watoto hawa walemavu, yatima, wanaoishi mazingira magumu na wenye mahitaji maalum wasiwe wanafikiwa tu kipindi cha Ramadhani, iwe ni utaratibu wa kila siku katika maisha yao yote."

Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, katika Iftar ya mjini Unguja, alisema SMZ inapongeza NMB kwa kudumisha utamaduni chanya wa kufuturisha wateja, sambamba na kusaidia watoto yatima na wanaoishi kwenye mazingira magumu visiwani humo, ikiwamo kuwaalika futari.

"Tunaishukuru Menejimenti ya NMB kwa kulifanya tukio hili kuwa endelevu, lakini mwaka huu mkaenda mbele zaidi kwa kutenga fungu la kununulia na kukabidhi misaada hii muhimu kwa watoto. Hakika mnastahili pongezi.

"Watoto hawa mnaowasaidia leo na wateja waliohudhuria Iftar hii na hata wale ambao hawakupata fursa hiyo, wataendelea kuheshimu na kuthamini huduma zenu," alisema Makamu wa Pili wa Rais.

Wakati wa Iftar iliyojumuisha watoto yatima wa vituo vya Zamzam na Darul Maarifu vya jijini Dodoma, Spika Dk. Tulia ambaye pia ni Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani, alisema NMB imefanya ibada kubwa kuwashika mkono watoto hao katika kipindi cha Ramadhan.

"Ni matumaini yetu kuwa kwa kazi nzuri mnayofanya NMB, ikiwamo kujali na kuthamini haya makundi maalum, mafanikio yenu yatakuwa makubwa zaidi na miaka ijayo tutashuhudia hafla hizi mikoani, kwa sababu Allah atakuongezeeni kutokana na ibada zenu za kujali wenye uhitaji," Spika Tulia alipongeza.

Vituo vilivyopatiwa msaada vikiwamo vya Al Zam Center (cha Mbagala Zakhiem, Dar), Umrah Center (Magomeni Mikumi, Dar) na Tanzania Kwanza Center (Kigamboni, Dar), navyo kwa nyakati tofauti vilitoa shukrani za dhati kwa misaada waliyopewa na NMB na kutaka agizo la Waziri Mkuu kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa lifanyiwe kazi.

# Majengo ya NHC yaanza kubomolewa Kariakoo

**Na Joseph Mwendapole**

MAGHOROFA 16 yanayomilikiwa na Shirika la Nyumba (NHC) katika maeneo ya Kariakoo, jijini Dar es Salaam, yameanza kubomolewa ili kuanza utekelezaji miradi ya ubia na kampuni binafsi utakaokuwa na thamani ya Sh. bilioni 271.

Katika ubomoaji huo ulioanza hivi karibuni, jumla ya maghorofa sita yameshabomolewa baada ya wabia kupata vibali vya ujenzi kutoka Manispaa ya Ilala, jijini na waliokuwa wapangaji wa shirika hilo kuhama.

Januari 29, mwaka huu, NHC ilitia saini mikataba na wabia hao mbele ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Jeryy Silaa katika ofisi za shirika hilo jijini, ambao watajenga majengo ya kisasa ya makazi na ya biashara kwenye maeneo yanayomilikiwa na shirika hilo.

Meneja Uhusiano na Mawasiliano wa NHC, Muungano Saguya, alimwambia mandishi juzi kuwa kadri wabia wanapopata vibali ndipo wanaanza kubomoa majengo hayo baada ya kuwapa wapangaji wanaotumia majengo hayo notisi ya mwezi mmoja kwa ajili ya kuhama.

Alisema mpaka sasa hakuna mgogoro wowote baina ya NHC na waliokuwa wapangaji wa maghorofa yaliyobomolewa kwa kuwa walishazungumza na kukubaliana kuhusu notisi watakayopewa na wanafahamu kuhusu utekelezaji mradi mzima.

Alisema wapangaji wote waliokuwa kwenye maghorofa hayo hawana malalamiko yoyote kwa NHC kwa kuwa walishakubaliana kwamba watapewa kipaumbele kurejea kwenye majengo hayo mara yatakapokamilika ndani ya miaka miwili au mitatu kuanzia sasa.

Akizungumza kwenye hafla ya kusaini makubaliano hayo Januari 29, mwaka huu, Waziri Silaa alipongeza NHC kwa mageuzi hayo makubwa waliyofanya kwa kuwa ujenzi utakapokamilika utaongeza idadi ya wapangaji kutoka 190 mpaka 2,011.

Alisema kwenye maeneo hayo kwa sasa kuna nyumba 72 lakini baada ya ujenzi zitaongezeka na kuwa 225 ikiwa ni mara tatu na nusu ya zilizopo sasa na aliwataka kuwapa kipaumbele wapangaji waliokuwa kwenye nyumba hizo mradi utakapokamilika.

Mkurugenzi Mkuu wa NHC, Hamad Abdalah Hamad, alisema shughuli za ujenzi zinatarajiwa kuanza mapema ambapo majengo 16 yatabomolewa kwa sababu wapangaji walishapewa notisi ya kuondoka.

Alisema miradi yote iliyoidhinishwa ina thamani ya jumla ya Sh. bilioni 271 kulinganishwa na thamani ya sasa ya majengo hayo ambayo ni Sh. bilioni 59.

Alisema miradi inayotarajiwa kutekelezwa itaongeza idadi ya nyumba za kuishi pamoja na maeneo ya biashara na hivyo kuchangia kutatua changamoto ya makazi bora na maeneo bora ya kibiashara.

Alisema miradi inayotarajiwa kutekelezwa eneo la Kariakoo itakuwa na jumla ya wapangaji 2,011 (maduka 1,258 stoo 500 na nyumba za makazi 253 kulinganishwa na idadi ya sasa ambayo ni wapangaji 190 (maduka 118 na nyumba za makazi 72).



# Waziri atishia kuwafuta kazi wakurugenzi mamlaka za maji

## -Bil. 600/- zahitajika kufunga mita malipo ya kabla

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

WAZIRI wa Maji, Jumaa Aweso, ametishia kuwatimua kazi wakurugenzi wa mamlaka za maji nchini ambao wataendelea kuzizoea shida za wananchi, hasa malalamiko ya kubambika ankara kubwa za maji ili kujipatia kipato.

Aweso alitoa hadhari hiyo jana akiwa katika Mji wa Moshi, mkoani Kilimanjaro wakati wa kikao kazi cha siku tatu na wakurugenzi watendaji wa mamlaka za maji Tanzania Bara.

"Tunakutana hapa kwa lengo la kujadili na kuweka mikakati ya kuboresha utoaji huduma bora za maji kwa wananchi. Sasa ninaagiza jikiteni katika kutatua kero zao zinazohusu maji, ambazo zimekuwapo kwa muda mrefu.

"Nitakutimua kazi wewe unayeona umezizoea shida za wananchi na hasa malalamiko ya kubambikiza bili za maji (ankara).

"Badilikeni na mwanze kutumia mifumo ya teknolojia kwenye kuboresha utoaji huduma za maji kwa wananchi ili kuleta mapinduzi kwenye sekta ya maji," aliagiza.

Waziri huyo pia alisema wizara yake imeanza kutekeleza maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan ya kuhakikisha taasisi na wananchi wanafungiwa mita za maji za malipo ya kabla kama mwarobaini wa malalamiko ya ubambikwaji wa bili za maji kwa wananchi.

Awali Mwenyekiti wa Wakurugenzi wa Mamlaka za Maji Nchini, Patrick Mzamba, alisema katika kikao hicho wamefanya tathmini na kubaini kuwa zaidi ya Sh. bilioni 615 zinahitajika kugharamia kampeni hiyo ya kufunga mita hizo za malipo ya maji kabla kwa wananchi na taasisi zote zilizoko Tanzania Bara.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Mwajuma Waziri, aliwataka wakurugenzi kuzingatia maadili ya utumishi wa umma, kuwasikiliza wananchi na kutatua kero zao kwa wakati.



Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa, Godfrey Mnzava (kulia) na Mkuu wa Wilaya ya Korogwe, William Mwakilema wakiwa wameushika Mwenge wa Uhuru 2024, wakiwaongoza wananchi kuukimbiza kwenye maeneo ya miradi wilayani Korogwe, mkoani Tanga jana. **PICHA: MASHAKA MGETA**

# Shirika la Australia lasaka suluhisho changamoto katika uzalishaji

**Na Godfrey Mushi,** ARUSHA

SHIRIKA la Kimataifa la Utafiti wa Kilimo la Australia limeanza mazungumzo na Shirika la World Vegetable Centre la mkoani Arusha, kutafuta suluhisho la changamoto katika uzalishaji mboga katika nchi zilizoko ukanda wa chini ya Jangwa la Sahara.

Mazungumzo hayo yanalenga kusaidia nchi 22 za Afrika Mashariki, Kusini pamoja na nchi kadhaa zenye uchumi unaokua kwa kasi kuinua sekta ndogo ya mboga ambayo imebaki kuwa isiyoendelea huku ulaji wa mboga nao ukiwa chini.

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la World Vegetable Centre wa Bara la Afrika, Dk. Gabriel Rugalema, alisema mataifa mbalimbali yanakuja Tanzania, kuiga mbinu za mafanikio kuwa na kanda za kilimo na nguvu kazi iliyo tayari kuzalisha mboga zenye ubora wa hali ya juu kwa matumizi ya masoko ya ndani na nje ya nchi.

"Worldveg inatengeneza aina za mboga zilizoboreshwa, mbegu na mfumo wa uzalishaji mazao na uhifadhi baada ya kuvuna ili kuhusisha wakulima kwa manufaa kwenye mnyororo wa thamani. Bidhaa na shughuli hizi zinachangia upatikanaji endelevu wa viini lishe kwenye mboga za gharama nafuu,"alisema.

Dk. Rugalema alisema Serikali ya Angola, imekubali kuingia makubaliano ya awali ya kushirikiana na World Vegetable Centre katika kujenga uwezo wa tasnia nzima ya mazao ya mboga, matunda, viungo na mazao mengine.

"Worldveg inatoa mafunzo ya uzalishaji mbegu bora kwa wakulima, mashirika ya mbegu, wataalamu wa mbegu na pia imeunda ushirika wa wazalishaji mbegu za mboga Afrika ili kuboresha mfumo mzima wa uzalishaji na usambazaji mbegu bora za mboga.

"Kitu kikubwa kinachovutia hawa ni regional harmonization kama za Afrika ya Mashariki na SADC (nchi zilizoko kusini mwa Jangwa la Sahara), kwani wanajifunza jinsi ambavyo kupitia hizi harmonization wanaona ni sehemu ya biashara kubwa ya mbegu katika ukanda wa Afrika ya Mashariki," alisema.

Asilimia 50 ya mbegu za nyanya na asilimia 98 ya mbegu za ngogwe zinazozalishwa kibiashara ndani ya Afrika ya Mashariki na kusini mwa Afrika, zinatokana na aina zilizotengenezwa na Kituo cha Worldveg.

Benki ya mbegu ya Worldveg iliyoko Arusha, kwa sasa ina aina za mbegu za mboga za asili 2,500, mfano mchicha, mlenda, ngogwe, mnavu, mgagani na nyinginezo.

Vilevile, Worldveg inakuza na kusambaza teknolojia ili kuongeza uzalishaji na matumizi ya mboga kwa kushirikiana na Kitengo cha Taifa cha Utafiti na Huduma za Ugani (NARES), asasi zisizo za kiserikali na sekta binafsi. Pia inakuza utafiti na maendeleo ya uzalishaji mboga na kutafuta suluhisho la matatizo ya uzalishaji mboga katika nchi zilizoko ukanda wa chini ya Jangwa la Sahara Afrika.

# Wataalamu waangalizi Mirerani wakwaa kashfa

**Na Mwandishi Wetu,** SIMANJIRO

WAMILIKI wa migodi ya madini ya Tanzanite iliyoko katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mirerani, wilayani Simanjiro, mkoani Manyara, wamewachongea kwa Waziri wa Madini, wataalamu waangalizi waliopelekwa na serikali katika eneo hilo kuangalia uzalishaji wake.

Wamemuomba Waziri Anthony Mavunde kuumulika mwenendo wa wataalamu hao, wakidai kuwa baadhi yao wanatuhumiwa kuingia katika migodi na kuchukua madini na kuyaficha.

Baadhi ya wamiliki hao kwa nyakati tofauti jana baada ya kuwapo ukakasi kuhusiana na matukio hayo, waliomba wasitajwe majina yao kwa sababu za kiusalama, walieleza:

"Haya madini wanachukua kabla ya kupelekwa kwenda kwenye tathmini; yanayopelekwa ni madini machache na yasiyokuwa na thamani na serikali kukosa mapato, kwa kuwa madini mazuri yamechukuliwa bila ridhaa ya mmiliki wa mgodi.

"Kutokana na yanayoendelea, tumeamua kumwandikia barua Waziri Mvunde (Waziri wa Nishati) kuhusu hali hii inayoendelea katika machimbo haya ya Mirerani."

Mmoja wa wamiliki hao wa migodi, alisema hali hiyo imekuwa kero kwao, ndiyo sababu iliyowasukuma kufikia hatua ya kufikisha malalamiko kwa Ofisa Madini Mfawidhi-Mirerani, lakini hakuna hatua yoyote hadi sasa inayochukuliwa.

Ofisa Madini Mfawidhi Mirerani, Nchahwa Chacha, alipoulizwa kuhusu madai hayo, alisema hana taarifa rasmi za malalamiko hayo.

Ni kweli wako wataalamu hao ndani ya ukuta wa migodi ya Tanzanite, ambao wako kwa kazi moja tu ya kusimamia uzalishaji na kufanya tathmini sahihi kwenye migodi unaozalisha madini na si vinginevyo.

"Mimi kama msimamizi mkuu wa migodi hiyo toka Wizara ya Madini, sina taarifa rasmi, na kama yapo malalamiko basi hayajanifikia ofisini kwangu. Niwatake wamiliki wa migodi ya Tanzanite kufikisha malalamiko yako ili nifanyie kazi," alisema.





# Wazazi walalamika magari shule binafsi kurundika watoto

**Na Restuta Damian,** KAGERA

BAADHI ya wazazi wenye watoto wanaosoma shule binafsi, mkoani Kagera wameiomba serikali kupitia Mamlaka za usafiri ardhini pamoja na usalama barabarani kudhibiti mienendo ya magari ya shule kurundika wanafunzi na kuhatarisha afya zao.

Walitoa kilio chao kwa nyakati tofauti wakati wakizungumza na Nipashe na kueleza kuwa utaratibu huo umekuwa ukisababisha watoto kurejea nyumbani wakiwa wachovu.

Irene Henerico, mkazi wa Kasharu, Manispaa ya Bukoba alisema alianza kugundua hali ya mtoto wake kubadilika kwa kurejea nyumbani akiwa mchovu kuliko kawaida na alipomuuliza sababu alimwambia ni kubananishwa kwenye gari la shule.

"Ni baada ya kuona hali imezidi kila siku, akaniambia kuwa kwenye gari lao wanakaliwa na watoto wanaowazidi umri ikiwa ni pamoja na kuzungushwa katika maeneo mbalimbali ambapo hadi wanafika nyumbani wanakuwa wamechoka zaidi," alisema Irene.

Tumain Pendamungu, Mkazi wa Kata ya Nshambya, Manispaa ya Bukoba, alisema huduma za shule binafsi upande wa masomo zinaridhisha isipokuwa upande wa kujali safari za watoto na kuomba serikali kufanya ufuatiliaji na kuweka utaratibu maalumu wa idadi ya watoto wanaotakiwa kuwa kwenye magari hayo.

"Pia kuna suala la watoto kuwawahisha shuleni ambapo wanaanza safari zao majira ya saa kumi na moja tofauti na kawaida ambapo watoto hawapati wasaa mzuri wa kusinzia na kupumzisha vichwa.Lingine ni suala la kuwaacha wavuke wenyewe nalo pia linahatarisha usalama wao barabarani tunaomba hatua zichukuliwe," alisema Pendamungu.

Mwenyekiti wa wamiliki wa shule binafsi Mkoa wa Kagera, Jay Jackson, alisema magari kwa shule hizo yapo kulingana na uwezo wa shule husika na kwamba ataendelea kuongea na shule zote kuhakikisha wanafunzi wanasafiri salama.

Alisema suala la watoto kuanza safari mapema ni takwa la Wizara ya Elimu kuwa vipindi vinatakiwa kuanza mapema na kueleza kuwa kama kuna upungufu mwingine wajitahidi kufahamishana ili wasisababishe madhara kwa watoto.

Mkuu wa Usalama Barabarani Wilaya ya Bukoba, Ramadhan Massimbo, alisema ni takwa la kisheria dereva kuwa na viti vinavyoendana na namba ya abiria alionao na pia wote kuhakikisha wanafunga mikanda.

Alisema kikosi hicho kinaendelea kusimamia sheria hizo kwa kuwachukulia hatua wote wanaokutwa na makosa kama hayo kwa kuwa hata magari ya shule yanatambulika kwa alama zake na yanafuatiliwa mara kwa mara kuhakikisha yanafuata sheria.

# Sherehe ya 'Birthday' yasababisha kifo

**Na Vitus Audax**

DAVID Deogratias, mkazi wa Ustawi, Kata ya Buzuruga mkoani Mwanza, anatafutwa na Polisi kwa tuhuma za mauaji ya Peter John (19) kwa madai ya vurugu zilizoibuka baada ya kumwagiana maji wakati wakisherehekea kumbukizi ya sikukuu ya kuzaliwa.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, DCP Wilibroad Mutafungwa, amethibitisha kutokea kwa tukio hilo ambalo lilitokea Aprili 4, mwaka huu wakati ndugu wote wakiendelea na sherehe hiyo.

DCP Mutafungwa alisema John (marehemu) alifikia nyumbani kwa Osombo Osombo (50), ambako sherehe hiyo ilifanyika ya kuzaliwa mjukuu wake Ester Musa aliyekuwa akitimiza mwaka mmoja.

Alisema wakiwa katika sherehe hiyo uliibuka ugomvi uliotokana na utaratibu wa kumwagiana maji na David Deogratias alichukia na kuamua kumchoma John kifuani na kitu chenye ncha kali maeneo ya chini ya ziwa upande wa kushoto na kusababisha kifo chake.

"John alifariki dunia wakati akiendelea kupatiwa matibabu katika Hospitali ya Rufani ya Sekoutoure na mwili umehifadhiwa katika hospitali hiyo kwa uchunguzi wa daktari na utakabidhiwa kwa ndugu kwa ajili ya mazishi," alisema.

Katika hatua nyingine DCP Mutafungwa alisema Jeshi hilo linachunguza kifo cha Riziwani Songora (45), mkazi wa Musoma, mkoani Mara kilichotokea Aprili 7 katika Bandari ya Mwanza Kaskazini.

Alisema Songora alifariki dunia akiwa njiani kupelekwa hospitalini na anadaiwa kuanguka na kutumbukia kwenye maji katika Ziwa Victoria ambako aliokolewa kabla ya kukutwa na umauti.

DCP Mutafungwa alisema mwili wa marehemu umehifadhiwa katika Hospitali ya Bugando kwa uchunguzi zaidi na utakapokamilika mwili utakabidhiwa kwa ndugu kwa ajili ya mazishi.

Alisema Jeshi hilo linaendelea kuimarisha ulinzi pamoja na usalama barabarani kuelekea Sikukuu ya Eid na kuahidi kuwachukulia hatua wote watakao jihusisha na vitendo vya uhalifu kwa kipindi hicho.



Baadhi ya wanafunzi wa Shule ya Msingi Lyasembe, Kata ya Murangi, Wilaya ya Musoma mkoani Mara, wakiwa nje ya darasa lao jana, lililoezuliwa paa kutokana na mvua kubwa ya upepo iliyonyesha mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wageni wadaiwa kusafirisha mchele nje ya nchi

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

BAADHI ya raia kutoka nchini Uganda wanaoingia nchini kwa vibali vya kusalimia ndugu zao, wamedaiwa kufanya biashara ya mchele kwa kupeleka nchini kwao kinyume cha sheria na taratibu hali inayosababisha bidhaa hiyo kuadimika wakati wa mavuno na wakulima kukosa chakula cha kutosha.

Madai hayo yaliibuliwa juzi na Mwenyekiti wa wafanyabiashara wa mchele, Kata ya Kagongwa Manispaa ya Kahama, Malando Dila, kwenye kikao kazi cha kubaini kero wanazokabiliana nazo kibiashara na kudai wananunua zao hilo moja kwa moja kutoka kwa mkulima shambani na kusafirisha kwenda nje.

Alisema, wafanyabiashara wengi kutoka nchi za jirani husuani Uganda wanaingia nchini na vibali vya kusalimia ndugu zao na muda mfupi wanaanza kununua mpunga kinyemela moja kwa moja kwa wakulima shambani badala ya kufuata sheria na taratibu za kibiashara.

Dila alisema, hali hiyo inasababisha wakulima kuuza mpunga wao kwa bei ya hasara ambayo haiendani na bei ya sokoni wakati huo na wanafanya hivyo kutokana na uelewa mdogo wa wakulima, huku wakiiomba serikali kuingilia kati na kuwadhibiti.

Katibu wa wafanyabiashara hao, Joseph Phabiani, alidai kuwa baadhi yao wanaingiza mchele wa Thailand kwa kutumia vibali wanavyopewa na serikali na kuuchanganya na mafuta ya elizeti ili kuubadilisha rangi na kisha kuufunga kwenye vifungashio vyenye nembo ya Tanzania na kwenda kuuza nje. Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Mboni Mhita akizungumza na Nipashe alithibitisha kuwapo kwa wafanyabiashara hao kutoka nchi jirani ambao wanawafadhili wakulima na kuwauzia baada ya mavuno hali inayosababisha kuuza kwa bei ya chini na kukosa chakula.

Kuhusu kuingizwa kwa mchele wa Thailand, Mhita alisema jumla ya wafanyabiashara watano wa ndani walikamatwa kwa kuchukua mchele huo na kuuchanganya na mafuta ya elizeti ili kubadilisha rangi ufanane na unaozalishwa nchini.

ALHAMISI APRILI 11, 2024

AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 12

**KUPITIA ULINZI KIAFYA...**

**Dk. Mpango asimulia wanavyoendeleza ubunifu wa Samia, kuwaibua mabinti**



Ukurasa 13

**SIKU YA AFYA DUNIANI**

Mwakilishi WHO asimulia walivyoshikamana na serikali kuisaka 'Afya Yangu, Haki Yangu'



Ukurasa 14

**Simulizi ya mateso na vitisho kuuawa katika ajira Uarabuni**

AFYA

# Treni SGR kuwa na 'hospitali ndogo' yenye huduma zote safari ikiendelea

**Na Beatrice Moses**

UWEKEZAJI uliofanywa na serikali kwenye ujenzi wa reli ya kisasa ya kimataifa (SGR), ili kuwa na usafiri wa treni ya kisasa inayotumia umeme(EMU), chini ya Shirika la Reli Tanzania (TRC), sasa unaonyesha mapinduzi makubwa.

Hapo kimsingi, unagusa sekta mbalimbali kama za usafiri, ajira, biashara, utalii na afya, ikiwa ni aina ya usafiri wa kisasa unaotarajiwa kuanza Julai mwaka huu.

Mhusika Mkuu, Shirika la Reli Tanzania (TRC), umeshatamka kujipanga vyema kuhakikisha huduma hiyo inakuwa ya kipekee, ikiwanufaisha wananchi kwa namna tofauti kama vile kiuchumi, kiutalii pia kiafya.

Katika sekta ya afya, ni usafiri huu unaotarajiwa pia kutumika kusafirisha wagonjwa wanaopata rufani ya kwenda kutibiwa kwenye hospitali kubwa mbalimbali, ambao mradi huo unahusika nako.

Hapo inajumuisha Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) iliyopo Dar es Salaam na kumeshaandaliwa utaratibu mzuri wa kuhakikisha wagonjwa wake wanasafiri salama.

Mganga Mkuu wa TRC, Dk. Peter Mganya, anaeleza kwamba huduma ya kwanza ya utabibu imekuwa ikitolewa hata kwenye treni ya kawaida, lakini kwenye hilo jipya wamekusudia kuiboresha kutokana na mazingira yalivyo.

"Treni ya SGR ina mwendokasi, pia haina mtikisiko. Hivyo, ni rahisi kumsafirisha mgonjwa hata anayepumua kwa kutumia gesi, kwa kuwa safari zake siyo za saa nyingi, tofauti na lile la MGR (la kawaida) ambalo inatumia saa nyingi na ina vituo vingi," anasema.



Huduma ya hospitali ya kisasa ikiendeshwa ndani ya usafiri wa treni ya kisasa (SGR), inayotarajiwa kuanza kazi hivi karibuni nchini. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

Dk. Mganya anataja malengo yao ni kuhakikisha wanawasaidia wanaopatiwa rufani, waweze kuutumia usafiri huo na tayari kuna wataalamu wa afya 20 waliopatiwa mafunzo maalum kufanikisha huduma hiyo.

"Tutazingatia taratibu za kusafirisha wagonjwa ikiwamo kujiridhisha kama hana ugonjwa wa kuambukiza hapa lazima kulinda, pia afya za abiria na wafanyakazi," anasema na kuongeza:

"Pia, mahitaji yake yatazingatiwa, kama anahitaji kutumia mipira ya chakula, au kupumulia mashine."

Anasema, wanatambua treni hiyo ya SGR kuwa mwendokasi tena kwa gharama za nauli kuwa za wastani, wakiamini wananchi wengi wenye wagonjwa wa rufani watautumia.

Mganga huyo anaendelea kuwa, treni ya kawaida kwa safari zake wamekuwa wakiwahudumia wagonjwa wa aina tofauti 30 kwa siku, hivyo ni wazi idadi hiyo itaongezeka.

Dk. Mganya anasema, wameshaweka utaratibu kwa kila kituo cha treni hiyo kutakuwa na mtaalamu wa afya anayesimamia kuhakikisha hali ya mgonjwa anayesafirishwa na mambo yanayopaswa kuzingatiwa.

"Pia tutakuwa na ushirikiano wa karibu na hospitali wanakokwenda wagonjwa husika, kwa kuhakikisha mgonjwa akifikishwa kwenye kituo anachoteremshwa, basi anapelekwa hospitali kwa utaratibu mzuri," anaeleza.

Hapo anaelezea hatua hizo, akitumkia kauli: "ikiwamo kutumia 'ambulance' (gari la wagonjwa) pale inapolazimu, ili mradi kuhakikisha mgonjwa anafika salama."

Kwa wajawazito, Dk. Mganya anasema, pia watajiridhisha kuwasafirisha katika namna inayowahakikisha wanabaki salama.

"Kwenye usafiri wa treni nasi tunazingatia taratibu kama vyombo vingine, hata katika kusafiri na abiria wajawazito.

"Nao watachunguzwa afya zao kabla ya safari, ili kuepusha kujifungulia ndani ya treni. Wanapaswa kupata huduma ya uhakika hospitali," anasema.

Mganga huyo wa TRC anaweka angalizo kwamba: "Simaanishi kwamba tunawaacha wajawazito tukiwakuta njiani hasa kwenye maeneo ambayo vituo vya afya vipo mbali, tutawapa huduma ya usafiri kulingana na mahitaji yao."

"Maana mwingine anaweza kuwa ndiyo anatumia usafiri wa treni kwenda ilipo hospitali kubwa, ili kujifungua," anasema.

Hadi sasa, usafiri huo aina mpya wa treni, tayari umeshafanya safari za majaribio kadhaa na sasa unatarajia kuanza kwa safari Dar es Salaam -Morogoro hadi Dodoma, itakayotumia saa tatu pekee.

Pia mganga huyo, anaeleza kwamba, tofauti na magari yanayotumia saa sita au zaidi, wao katika treni ya SGR wanatarajia kuwa na urahisi zaidi wa kusafirisha mgonjwa, pale inapobidi.

**INAENDELEA UK.12**

AFYA

KUPITIA ULINZI KIAFYA...

# Dk. Mpango asimulia wanavyoendeleza ubunifu wa Samia, kuwaibua mabinti

• Waziri Ummy na siri mafanikio 'mtaani' kwake

**Na Yasmine Protace**

KATIKA nyendo zake za kiuongozi na kisiasa, daima amekuwa hawasahau kinamama, akitetea jinsia yake, ambayo pia ni ajenda ya kitaifa na kimataifa.

Akigawanya katika sura kuu mbili; eneo moja ni kinamama watu wazima ambao pia ni wazazi na bibi, huku upande wa pili ni kwa walio watoto - mabinti.

Ni katika kundi hilo la Watoto, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, ndani ya zama za uongozi wake wa urais akiwa mwaka wa tatu, amekuja na zawadi kubwa kwa mabinti masomoni.

Mnamo mwezi Machi mwaka huu, akiwa jijini Dodoma, Rais Dk. Samia akatangaza hatua ya kuanza kutekelezwa ujenzi wa shule maalum za bweni kwa wasichana.

Ni mradi unaotazama ujenzi wa shule 26, kila mkoa shule moja kwa gharama ya Sh. bilioni nne kila moja, na serikali ikianza kutoa fedha hizo, ili kutoa fursa kwa wanafunzi wa kusoma kwa ufasaha kuelewa kwenye mafanikio yao nchini.

Hiyo ni kupitia Mradi wa Kuboresha Elimu ya Sekondari (SEQUIP) wa Miaka mitano, serikali ikilenga kutenga Sh.trilioni 1.2 kwa ajili ya kujenga shule mpya za sekondari 1,026 na kati ya hizo, shule 26 ni maalum za wasichana.

Hiyo ikatajwa itawezesha shule hizo maalum kupokea wanafunzi 1,080 wa kidato cha kwanza hadi cha sita.

Kinadharia inatangazwa, mtoto wa kike anaposimamiwa ipasavyo, ikiwamo kutambulika haki zake, kunampatia matunda, huku wakitakiwa kusimamiwa katika kupata haki zao.

Hiyo inatokana na malalamiko katika baadhi ya maeneo watoto wa kike wamekuwa wakikosa haki tajwa, hata wanashindwa kuyafikia malengo yanayotakiwa, hasa pale usimamizi stahiki unapokosekana.



Makamu wa Rais Dk. Philip Mpango, wakati wa hafla ya ufunguzi wa Kongamano la Wanawake la Nishati Safi ya Kupikia iliyofanyika, Jijini Dodoma. **PICHA: MTANDAO.**

### MAKAMU ANAVYOENDELEZA

Hivi karibuni, Makamu wa Rais nchini, Dk. Philip Mpango katika kuendeleza falsafa na hatua za mkuu wa nchi, akatamka haja ya umma kuwa mstari wa mbele kusukuma ajenda za kumkomboa mtoto wa kike, dhidi ya changamoto zinazomkabili.

Ni kauli yake Dk. Mpango, katika ufunguzi wa mkutano kimataifa wa masuala ya uongozi kwa wanawake kisekta, uliofanyika mjini Dar es Salaam.

Anasema, hatua iliyofikiwa ni kwamba uwekezaji mkubwa umeshafanywa kwenye sekta za afya, maji, elimu na nishati, zikiwa na jitihada za makusudi kumuinua mtoto wa kike, kutokana na kuwa na changamoto zinazowakabili kwa muda mrefu.

Hapo kuna mambo yanayotajwa kama vile; mila potofu pamoja na mfumo dume uliokuwa umeshamiri miongoni mwa baadhi ya jamii.

"Jitihada hizo upande wa sekta ya afya, kupitia huduma inayotekelezwa na mpango wa 'M-Mama' umewezesha kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi, kutoka 556 kwa kila vizazi hadi 100,000 mwaka 2016 hadi kufikia vifo 104 kwa kila vizazi hai 100,000 kwa sasa." anasema.

Anaeleza katika sekta ya maji, Rais Dk. Samia amejitahidi 'kumtua mama ndoo kichwani' kwa kuhakikisha huduma ya maji inapatikana kwa uhakika, ikifuta adha kwa mwanamama, kufuata maji umbali mrefu.

Hapo anatoa takwimu kwamba, katika bajeti ya maji imepaa akitumia mfano wa Sh.bilioni 709.4 kwa mwaka wa fedha 2022/23 hadi Sh.bilioni 756.2 bajeti iliyopo sasa.

Makamu wa Rais anasema, serikali chini ya Dk. Samia imedhamiria kuwa na nishati safi na salama kwa mazingira salama kwa jamii, akinena shabaha ya serikali ni kuhakikisha ifikapo 2030, matumizi ya nishati safi na salama kwa mazingira, inafikia asilimia 80, husussan ni maeneo ya vijijini ambako matumizi ya nishati isiyo rafiki iko juu.

Katika sekta elimu, Dk. Mpango anataja jitihada zilizopo zina tija kwa watoto wa kike kujengewa shule maalumu za bweni, ili waweze kuhitimu masomo yao na kufikia matamanio yao ya kile wanachotaka kufanya maishani.

"Wapo baadhi ya watoto wa kike walikuwa wamepata ujauzito na kujifungua watoto, serikali ya Dk. Samia Suluhu Hassan imehakikisha, wanarudi shuleni hata baada yakujifungua na kuendelea na masomo," anasema.

### ANENAYO WAZIRI UMMY

Kwa upande wake Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, akasifu mjumuiko huo, akiutaja mkutano uliopo umekuwa ni heshima kwa nchi kupokea, kwani ni kwa mara ya pili unafanyika katika bara la Afrika, awali ulifanyika nchini Rwanda.

Anataja sababu akisema: "Ni kutokana na nchi kufanya vizuri katika viashira vikuu vya kupima afya duniani, kwani kama nchi tumeweza kupunguza vifo vya mama wajawazito kwa hadi asilimia 80.

Anaendelea: "Kwani, mbali ya kupunguza vifo vya vizazi hai lakini pia kwa upande wa vifo vya watoto wa chini ya miaka mitano kutoka vifo 67 hadi vifo 45 kati vizazi 1000."

Anaeleza kuwa wasifu walio nao viongozi wake akiwamo Rais Dk. Samia na makamu wake, aliyekuwa mgeni rasmi katika hafla hiyo, ni; nguvu, ujasiri, usemi na msikilizaji.

Hapo anasema, kiongozi huwa unagusa maisha ya watu katika ngazi zote kama vile Rais wake, wabunge na mawaziri.

INAENDELEA UK.14

## Treni SGR kuwa na 'hospitali ndogo' yenye huduma zote safari ikiendelea

INATOKA UK.11

Mganga huyo wa TRC anaweka angalizo kwamba: "Simaanishi kwamba tunawaacha wajawazito tukiwakuta njiani hasa kwenye maeneo ambayo vituo vya afya vipo mbali, tutawapa huduma ya usafiri kulingana na mahitaji yao."

"Maana mwingine anaweza kuwa ndiyo anatumia usafiri wa treni kwenda ilipo hospitali kubwa, ili kujifungua," anasema.

Hadi sasa, usafiri huo aina mpya wa treni, tayari umeshafanya safari za majaribio kadhaa na sasa unatarajia kuanza kwa safari Dar es Salaam –Morogoro hadi Dodoma, itakayotumia saa tatu pekee.

Pia mganga huyo, anaeleza kwamba, tofauti na magari yanayotumia saa sita au zaidi, wao katika treni ya SGR wanatarajia kuwa na urahisi zaidi wa kusafirisha mgonjwa, pale inapobidi.

Dk. Mganya anasema, usafiri wa treni unabaki kuwa wa uhakika, usio na ajali zaidi, ikilinganishwa na magari ya kawaida, hivyo watu wengi ambao reli imepita katika maeneo yao wanavutiwa na 'mgeni' SGR.

Pia, treni hiyo inatajwa kuwa mpya kwa aina yake, hivyo wanaamini inaangukia kwenye kivutio.

Mkurugenzi Mkuu wa TRC, Masanja Kadogosa, anatolea ufafanuzi kwamba, tayari wao walishanunua mabehewa 89 ya abiria na vichwa 19 vya EMU, pia vifaa vya kisasa vya matengenezo ya njia 24.

Kimsingi, Bunge nchini limeshaidhinisha TRC kupitia Wizara ya Uchukuzi, kwamba ipewe fedha Sh. trilioni 1.113 katika bajeti ya fedha iliyoko sasa, mwaka 2023/2024.

Maudhui yake ni kugharamia ujenzi wa reli ya kimataifa kununua mabehewa, abiria na mizigo na kugharamia upembuzi yakinifu.

Vilevile, ni fedha hizo zilizoidhinishwa kugharamia uendelezaji mafunzo kwa wataalamu wanaoendesha na kusimamia treni hiyo ya EMU.

AFYA

SIKU YA AFYA DUNIANI

# Mwakilishi WHO asimulia walivyoshikamana na serikali kuisaka 'Afya Yangu, Haki Yangu'

• Safari ya chanjo, tiba, NCD, maambukizi hatari...

**Na Dk. Charles Sagoe - Moses**



Dk. Charles Sagoe-Moses (kulia), Mwakilishi wa Shirika la Afya Duniani (WHO), akiwa katika wodi ya uzazi katika Hospitali ya Mnazi Mmoja, Zanzibar. **PICHA: WHO**

KILA mwaka inapotimu siku ya Aprili 7, Shirika la Afya Duniani (WHO), linaungana na wanachama wa Umoja wa Mataifa (UN), pia mashirika, jumuiya za kimataifa na kitaifa wakiadhimisha siku hiyo.

Hiyo ni fursa kwa dunia kujielekeza na kuweka msisitizo, umakini kwa umma kuhusu masuala ya afya na kuendeleza ajenda ya Chanjo na Afya kwa Wote.

Ujumbe wa mwaka uliopo ni 'Afya Yangu, Haki Yangu', ikimaanisha kuhakikisha kila mtu ana haki hiyo kupata huduma ya afya popote, elimu, taarifa pamoja na maji salama na safi ya kunywa.

Pia, ujumbe wa mwaka huu unahimiza haki ya kuwa na hewa safi, lishe bora, makazi bora, kazi yenye hadhi, mazingira mazuri, kuwa huru na kuondokana na ubaguzi.

## AFYA YANGU, HAKI YANGU

Dunia hadi sasa imezama katika majanga mengi, kama vile migogoro inayosababisha kuwapo kwa hali za dharura kimazingira, mamilioni ya watu wakitengwa duniani na wengine wanateseka.

Katika kushughulikia na kukuza afya kama haki ya binadamu, kunahitajika msisitizo kijamii, kiuchumi na kimazingira, ili kuleta matokeo chanya.

Hilo linamaanisha kukuza, haja ya usawa wa kijinsia unaohakikisha upatikanaji wa maji safi na usafi wa mazingira, huku kuna kukabiliana na Sababu Kuu za Utapiamlo na Magonjwa Yasiyoambukiza (NCDs).

Ndani yake pia kuna, haki ya kufikia kiwango cha juu zaidi cha afya ya kimwili na kiakili, imewekwa na kutambuliwa na vyombo kadhaa vya kisheria vya kimataifa, ikiwamo Mkataba wa Kimataifa wa Kiuchumi, Kijamii na Kiutamaduni.

Haki hizo inajumuisha uhuru na haki. Uhuru huo unajumuisha haki ya kudhibiti afya na mwili wa mtu na kuwa huru kutoingiliwa. Kwa mfano ni kuishi bila mateso, matibabu na majaribio (hasa kiafya) yasiyo ya ridhaa, hasa kwa watu wenye ulemavu.

Hiyo ni katika kuheshimu haki ya afya, kuheshimu haki yetu ya afya kukimaanisha; kuheshimiwa haki zetu za kupata maji safi ya kunywa, hewa safi, lishe bora, makazi bora, mazingira mazuri ya kazi na uhuru dhidi ya migogoro na ubaguzi.

## AJENDA KIAFYA KITAIFA

Hadi sasa, Tanzania inaendelea kujitahidi kufikia afya kwa ajenda zote, kwa kuzingatia haki za kila mtu na kuhakikisha inaingizwa katika sera na afua.

Katika mustakabali huo, WHO, pamoja na serikali na washirika wengine wanaonyesha dhamira ya pamoja isiyoyumba ya 'Afya kwa Wote'

iliko, WHO inashirikiana sasa na serikali kuchunguza njia za kuimarisha mifumo ya afya, kuboresha kufikiwa huduma muhimu za afya na kukuza ujuzi wa kusoma na kuandika na uhamasishaji wa afya.

Mnamo Mwaka 2022, ofisi ya WHO nchini, kwa kushirikiana karibu na wadau, iliandaa mpango wa Mkakati wa Ushirikiano wa Nchi (CCS) wa miaka sita (2022-2027).

Huo ni mkakati wa mfumo wa pamoja na WHO katika kukidhi mahitaji na vipaumbele vya nchi, kulingana na Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) ya 13 yanayohusiana na afya, ikitoa mfumo wa ushirikiano wa kimkakati wa muda wa kati kwa WHO katika kufikia vipaumbele vya kimkakati vya afya ya Tanzania.

Pia, hapo kuna suala la muda unaotokana na Mfumo wa Ushirikiano Endelevu wa Umoja wa Mataifa (UNSDCF) kwa Tanzania, huku vipaumbele vyake vinawiana na Mpango Mkakati wa Kitaifa wa Sekta ya Afya, SDGs, GPW13 na UNSDCF.

Kwa msaada kutoka kwa washirika wengine, WHO Tanzania ina msimamo wa kuendelea kusaidia nchi katika midahalo ya kimkakati na kisera.

Hapo mkakati uliopo ni kusaidia kudumisha mfumo wa afya unaoweza kutoa huduma inayofikiwa, nafuu, yenye ubora, kamili na iliyounganishwa kwa ajili ya huduma ya afya kwa wote na usawa wa afya, sambamba na 'Ajenda ya 2030 ya Maendeleo Endelevu.'

Kupitia kushughulikia milipuko mikuu ya kiafya kama vile maradhi ya Uviko-19, virusi vya Marburg, kuna hatua zinazoendelea kuimarisha utayari, kupitia ujenzi wa uwezo na mafunzo kwa wafanyakazi wa afya na kufadhili vituo vya afya, ili kufaa kwa madhumuni.

## KUPUNGUA VIFO UZAZI

Inatajwa kwamba ni ngumu kuzungumzia mafanikio makubwa nchini, pasipo kutaja kupungua kwa vifo vya uzazi, jitihada za kumfikia kila mtoto na chanjo, kushughulikia maradhi kama Ukimwi na kusambaa virusi vya - VVU, kifua kikuu, homa ya ini, malaria na maradhi yasiyoambukiza, kama vile mapigo ya juu na chini ya moyo.

Hata hivyo, kazi za yanayolengwa kufanikiwa afya bora haijakamilika. Ili kutimiza maono ya afya kwa wote na kuendeleza haki za mtu binafsi kupata huduma za afya, kunatajwa haja ya juhudi za kushughulikia viashiria vya msingi vya afya, ikiwamo kupinga umaskini, kukosena usawa kijamii na miundombinu duni.

Ndiyo hapo kunakopatikana ulazima wa kuendeleza uwekezaji katika huduma za afya ya msingi na huduma za kijamii, ili kuhakikisha hakuna anayeachwa nyuma

> "Mnamo Mwaka 2022, ofisi ya WHO nchini, kwa kushirikiana karibu na wadau, iliandaa mpango wa Mkakati wa Ushirikiano wa Nchi (CCS) wa miaka sita (2022-2027).

## USHIRIKIANO KATIKA AFYA

Katika eneo hilo, kunatajwa haja ya kuwapo ubia wa kimkakati, kwa ajili ya ajenda ya afya nchini, ikiangaliwa, suala la kuwapo utawala unaojitolea 'kuelekea ajenda ya afya' kunaonekana maslahi makubwa na uwekezaji, lakini kuna nafasi zaidi ya kuboresha.

Eneo lingine linatajwa bado halijatumika, ni katika ushiriki wa jamii na raia. Ingawa bado ni changamoto kubwa, ushiriki wa kijamii, yaani kushirikisha umma katika kufanya maamuzi ya afya kupitia mikutano, makusanyiko ya wananchi, makundi lengwa na mashauriano, mabaraza ya afya, na uwakilishi kwenye vikundi vya uongozi na bodi za mapitio.

Hiyo inatajwa inaisaidia serikali kutathmini mahitaji ya afya na idadi ya watu na kuyafanyia kazi, ili kupanua ufikiaji wa huduma bora za afya na kuruhusu kila mtu, kila mahali kuishi maisha yenye afya.

WHO wakiwa wadau, wanahimizwa kuwekeza katika afya, kwani msingi wa nchi unategemea hilo, kwa sababu raia wenye afya na nguvu inamaanisha nguvu kazi na nguvu kazi iliyo tayari kukuza ukuaji wa nchi.

***• Mwandishi wa makala hii ni Mwakilishi Mkazi wa Shirika la Afya Duniani (WHO), Tanzania.***

AFYA

# Simulizi ya mateso na vitisho kuuawa katika ajira Uarabuni

**Na Mwandishi Wetu**

IRENE Lavender (25) mwanamke kutoka Kenya, aliyeondoka nchini mwake miaka mitatu na nusu iliyopita kutafuta maisha nchini mwake, huko akakutana na mazito kimaisha.

Irene anasema baada ya kukamilisha elimu ya sekondari hakupata ajira, wakati huo familia yake haikuwa na uwezo kumwendeleza kielimu.

Ndipo Irene, akaamua kutafuta kazi za nyumbani nchini Misri mwaka 2020. Anasimulia: "Nilipowasili Misri nilikuwa na msisimko wa kuzuru nchi nyingine. Nakumbuka pia siku hiyo mvua ilinyesha sana... ila ilibidi nivumilie.

"Siku moja baada ya kuwasili, Misri ulitangazwa mlipuko wa Covid 19, hivyo basi kulazimisha mambo mengi kusimama. "

Irene anasema akapata ajira ya kwanza Misri kwa jamaa mmoja tajiri. Anasema ilikuwa mara ya kwanza kufanya kazi za ndani, hivyo basi uzoefu wake ulikuwa mdogo wakati huo.

Mwajiri wake mwanzoni, alikuwa amemueleza kuwa kazi zake zitahusu kuwatunza watoto pekee na kumficha kwamba angehusika na kazi za ziada kama usafi na kufua.

"Jambo la kuridhisha ni kuwa watoto wa familia hiyo walinipenda sana na kwa uzoefu wa kufanya kazi Uarabuni, iwapo watoto wa familia wangekuwa na urafiki na mfanyakazi basi alikubalika kwa urahisi.

"Changamoto kuu niliyokuwa nayo ya kazi sikuwa na uzoefu wa kufanya kazi katika nyumba kubwa, nikiifananisha na kasri" anaeleza.

Baada ya kufanya kazi huko kwa wiki kadhaa Mwanamke aliyekuwa mwajiri wake Irene, alianza kumzaba makofi, pia kumchapa kwa kila kosa.

Anatoa mfano, hakuwa na uzoefu wa kutumia mashine zinazotumia umeme kufua, kuosha vyombo na hata za kupikia, hivyo basi akashindwa kuzitumia bila ya muongozo sahihi, ambao hakupata wakati wa kuajiriwa kazi .



Irene Lavender. **PICHA: MTANDAO**

Irene anasema, pia mwajiri wake alimshurutisha kufanya kazi saa 12, akimaanisha kuwa kuna siku alisimama jikoni kuanzia saa12.00 jioni hadi saa 12 siku inayofuata.

Anasema, hilo lilifanyika huku mwajiri wake akiwa amemsimamia na kukagua kila kitu alichomuamrisha kufanya usiku huo, akimaanisha kuwa hakulala usiku kucha.

Cha kuzidisha uchungu kwenye kidonda Irene anasema, mume wa mwajiri wake alikuwa na tabia za kumtomasa na kumshika kila wakati akiwa jikoni, huku akimwahidi kumpa pesa iwapo angesalia kimya kuhusu hali hiyo.

"Kila wakati alipokuwa ananishika yule mwanaume alikuwa ananipa pesa, mimi nilizichukua kwani nilijua siku moja pesa hizo zingenisaidia kutoroka katika makao hayo kwani tayari nilikuwa nimechoka," anasema.

Mwanamke huyo anaeleza kisa cha mwisho kilichomfanya atoke kwenye makao hayo, ni kosa alilofanya la kutumia mashine ya kuosha vyombo , hata mwajiri wake kumtishia kumchoma kisu, ila mume wa muajiri huyo akamuokoa kutoka patashika hiyo.

Baada ya hapo Irene, anasema akaamua kutoroka kutoka makao hayo kwa usaidizi wa binamu yake aliyekuwa pia mjakazi huko Misri.

## NYUMBA YA PILI

Irene anasema, akafanikiwa kupata ajira nyingine kwenye makao mapya huko Misri , kazi yake kuu ilikuwa kutunza watoto mapacha , na wakati mwingine kupakuwa chakula kwa jamii hiyo .

Katika makao hayo, mwanadada huyu anasema kuwa mwanzo kila kitu kilikuwa shwari na hakuwa na shida na mwajiri wake, akikumbuka ukarimu wake kiasi kwamba akaahidi kumrejesha chuo kikuu kwa mafunzo maalum, jambo ambalo halikufanyika.

Irene anasema, mwajiri wake alikuwa na imani naye hasa kwa kuwa alikuwa na bidii ya kuwatunza watoto wake kama ilivyohitajika.

Ila anasema mwajiri wake (mama wa nyumba) alianza kubadilika baada ya miaka miwili hivi, siku moja Irene anasema kuwa alisingiziwa kuwa alihusika na wizi wa mkoba maalum wa thamani, ambao ulikuwa wa mwajiri wa kike.

Ni jambo anataja lilimkasirisha mwanadada huyo na wakati wa likizo aliamua kuacha kazi katika makao hayo, licha ya kuwa iligunduliwa kuwa yeye hakuhusika na kupotea kwa mkoba huo.

"Baada ya miezi mitatu nilipokea simu kutoka kwa mwajiri huyo huyo akinisihi nirejee kazini, nilimpa mwajiri wangu mazingira ya kurejea kazini ilikuwa ni iwapo atajadili swala la kusingizia kuwa nilihusika na wizi wa mkoba wake, aliridhia na kusema kuwa sio mimi niliyehusika, vile vile alinongeza mshahara na ndipo sasa nikakubali kurejea huko," anakumbusha Irene

Haikuchukua muda tena na mwanadada huyo anadai kuwa mwajiri wake alianza madai mapya kuwa mwanadada huyu alikuwa amehusika na wizi wa pete zake za dhamana kubwa.

Irene anasema kwa kipindi cha siku moja walishurutishwa kama wafanyakazi kuitafuta pete hiyo mchana kutwa, wakati huo wote Irene anasema kuwa mwajiri wake alitishia kuwa iwapo pete hiyo haingepatikana angechukuliwa hatua mbaya.

"Mwajiri wangu aliwaita wanaume wawili kwa kile alichokisema kuwa naadhibiwa ili niseme nilipoficha pete zake, wanaume hao walinivua nguo zote huku wakisaka pete hio mwilini mwangu.

Kitendo hiki kilinidhalalisha mno na kunipa aibu ambayo sitawahi kuisahau milele ."anakumbuka Irene

Ilipoonekana kuwa Irene alisimamia kidete kuwa hakuhusika na wizi huo, mwajiri wake aliwaachilia wanaume waliohusika na dhuluma , na akawasilishwa mikononi mwa polisi .

Irene anasimulia siku zilizojaa kiza kikuu ndani ya jela alikofungiwa huku akishurutishwa kusema alipoficha pete ya mwajiri wake.

Hali ikaendelea kuwa mbaya hadi alipowasilishwa mahakamani na jaji akaamua kuwa hatma ya Irene ilikuwa arejeshwe nchini mwake mara moja .

Irene alirejeshwa Kenya mwezi Machi mwaka huu. Mwanadada huyo sasa anasema kuwa amesoma mengi kuhusiana na masaibu yake nchini Misri, akitoa nasaha kwa wanaotafuta ajira nje ya nchi kwanza kuchunguza mazingira wanayopania kufanya kazi na pia kuwa na watu wa karibu wanaoweza kuwafahamisha iwapo kutatokea dharura.

• ***Kwa mujibu wa BBC***

# Dk. Mpango asimulia wanavyoendeleza ubunifu wa Samia, kuwaibua mabinti

**INATOKA UK.12**

Anaeleza kuwa wasifu walio nao viongozi wake akiwamo Rais Dk. Samia na makamu wake, aliyekuwa mgeni rasmi katika hafla hiyo, ni; nguvu, ujasiri, usemi na msikilizaji.

Hapo anasema, kiongozi huwa unagusa maisha ya watu katika ngazi zote kama vile Rais wake, wabunge na mawaziri.

Anasema, katika mkutano huo ajenda kuu tatu za kujadiliwa zilijumuisha; uongozi wa mabadiliko, ushirikiano kama njia ya usawa wa kijinsia, na hatua za kuendeleza uongozi wa wanawake kwenye sekta ya afya zinazoendana vyema, pia uongozi wa mabadiliko kama za Rais Dk. Samia.

Aidha, Waziri Ummy anasema katika uongozi wa Rais Dk. Samia, ambaye ni mwanamke, pia yeye akiwa mwanamke waziri, pia anayemsaidia rais katika eneo la afya, Tanzania imepunguza vifo vya kinamama wajawazito kwa zaidi ya asilimia 80 kutoka vifo 556 hadi vifo 104 katika kila vizazi hai 100,000.

"Pia, Tanzania imeweza kupunguza vifo vya watoto wenye umri chini ya miaka mitano kutoka vifo 67 katika kila vizazi hai 1,000 hadi vifo 43 katika kila vizazi hai 1,000.

"Kwa sasa tunakwenda kuboresha huduma za Afya na kuhakikisha tunapunguza vifo vya watoto wachanga wenye umri wa siku sifuri hadi 28". anasema.

Kwa upande wake, Verda Msangi, mjumbe katika mkutano huo, akataja utayari wao kujifunza kutoka kwa wanawake wengine viongozi, kwa kuwa wanaweza kuingia kwenye nafasi za uongozi kama ilivyo kwa Waziri Ummy.

"Tupo hapa pia kujifunza na kuona jinsi gani tutashirikiana ili kuhakikisha Afya ya Mwanamke na Afya za Watanzania zinaweza kuimarika kupitia mashirikiano hayo na mahusiano," akahitimisha.





# Serikali kuanzisha tuzo ya uandishi vitabu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KATIKA kukabiliana na uchapishaji wa vitabu vya watoto visivyo na maadili, Serikali imekuja na mkakati wa kuanzisha tuzo ya uandishi wa vitabu vinavyoendana na maadili ya kitanzania, ili kuimarisha upatikanaji wake.

Machi, 2023, Serikali ilipiga marufuku baadhi ya vitabu vya watoto vilivyobainisha kukinzana na mila, desturi, miongozo na tamaduni za mtanzania.

Akizindua jana jijini hapa kuhusu wiki ya kitaifa ya elimu, ujuzi na ubunifu 2024 yatakayofanyika mkoani Tanga Mei 25-31 na hafla ya utoaji wa tuzo ya taifa ya Mwalimu Nyerere ya uandishi bunifu itakayofanyika Aprili 13, mwaka huu, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, alisema tuzo hiyo inalenga kuchochea uandishi vitabu nchini.

"Tumeongeza uandishi wa vitabu vya watoto, mtakumbuka siku moja tukaeleza hapa vitabu ambavyo tumetumia mamlaka ya kisheria kuviondosha shuleni kwasababu vilikuwa vinaingiza masuala yanayokinzana na maadili yetu."

"Kuondosha vitabu inaweza kuwa rahisi lakini tunapeleka nini shuleni na vitabu vya namna gani, tungependa viandikwe vitabu vyenye kufurahisha vinavyopendwa ili kuziba ombwe la kutokuwa na vitabu vya kutosha," alisema.

Alisema hatua hiyo itaongeza uchapishaji wa vitabu nchini kwa kuwa kampuni za uchapishaji zipo hatarini kufa kutokana na kukosa biashara.

Katika hatua nyingine, akizungumzia maadhimisho ya wiki hiyo, Prof. Mkenda alisema katika kipindi cha mwaka 2019 hadi 2023, zaidi ya bunifu 2000 zimetambuliwa na kati yake 283 zinaendelezwa na 42 zimefikia hatua ya kubiasharishwa.

Alisema maadhimisho hayo yanatoa fursa kwa wabunifu kuonana na wawekezaji watakaochangia kubiasharisha matokeo ya utafiti na bunifu zao.

"Bunifu 42 zipo sokoni na zinatumika kutatua changamoto za maji, kilimo, nishati, afya na elimu, maadhimisho ya mwaka huu yatahusisha maonesho ya bidhaa na teknolojia mbalimbali," alisema.

Alisema dirisha la usajili Mashindano ya Ubunifu wa Sayansi na Teknolojia (MAKISATU) limefunguliwa jana na litafungwa Mei 8, 2024 na kutoa wito kwa wabunifu kujitokeza kwa kuwa kupitia mashindano hayo watapata fursa ya kwenda kushiriki kidunia.



Madaktari Bingwa kutoka hospitali mbalimbali za Jiji la Dodoma (kulia), wakiwapima shinikizo la damu wananchi waliojitokeza kwenye kambi ya siku moja ya upimaji wa afya bure katika kata ya Mpunguzi, jijini humo, hivi karibuni. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Waziri atoa maagizo TANROADS barabara zilizoathiriwa na mvua

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

NAIBU Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Zainab Katimba ameagiza Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA) kuendelea kuchukua hatua za kurejesha barabara zilizoathiriwa na mvua, ili wananchi wasikwame kwenye shughuli zao za kiuchumi.

Katimba aliyasema hayo jana alipotembelea makao makuu ya TARURA jijini Dodoma na kupokea taarifa ya utendaji wa kazi za wakala huo.

Alisema barabara zinachangia katika uchumi na ustawi wa maisha ya watu.

"Hizi ndizo barabara wakulima wanatumia kusafirisha mazao yao, katika kipindi hiki cha mvua maeneo mengi hususani vijijini yanaathirika na hatua za dharura zinapaswa kuchukuliwa ili kurejesha mitandao ya barabara na kuwapa wananchi fursa ya kuendelea na shughuli zao za uchumi," alisema.

Alisema Rais Samia Suluhu Hassan ameongeza bajeti ya TARURA kufikia Sh. bilioni 710 kutoka Sh. bilioni 275 kutokana na umuhimu wa barabara za wilaya ambazo ni nyenzo kuu ya uchumi wa wananchi.

"Serikali inatambua kuwa upo uhitaji mkubwa wa ujenzi na uboreshaji wa barabara zilizo chini ya TARURA ni jukumu lenu kutekeleza majukumu yenu kwa uadilifu ukizingatia matarajio ambayo jamii inayo juu yake.

Alisema uharaka na ubunifu wa utatuzi wa kero za dharura zinapojitokeza ni jambo muhimu la kuzingatiwa na wakala huo.

Naye, Mtendaji Mkuu wa TARURA, Victor Seff alisema kuwa kazi kubwa inafanyika kurejesha mawasiliano ya barabara zilizoharibiwa na mvua inayoendelea kunyesha.

Alisema: "Kwa sababu rasilimali fedha bado haitoshi tunajitahidi kuelekeza nguvu katika maeneo yenye umuhimu zaidi yanayounganisha huduma za kijamii kama shule na hospitali".

# Magereza, REA zakubaliana matumizi nishati safi

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

JESHI la Magereza nchini limeingia makubaliano na Wakala wa Nishati Vijijini (REA) wa matumizi ya nishati safi katika magereza 129 ili kuepuka uharibifu wa mazingira.

Akizungumza kwenye hafla ya utiaji saini mkataba huo jana wenye thamani ya Sh. bilioni 34.9, Mkuu wa Jeshi la Magereza nchini, Kamishna Jenerali Ramadhan Nyamka alisema jeshi hilo linakwenda kuachana na matumizi ya kuni katika kupikia.

"Tunawashukuru sana REA kwa kuingia mkataba nasi niwahakikishie nishati safi itaendelea kutumika katika magereza yetu mbalimbali hapa nchini,"alisema.

Alisema nishati safi itarahisisha pia katika maandalizi ya vyakula vya magereza na itafanya wapike kwa kutumia muda mfupi, tofauti na ukitumia kuni.

Naye, Mkurugenzi wa REA, Hassan Said alisema wataendelea kutoa ushirikiano kwa jeshi hilo ili kuhakikisha wanatumia nishati safi.

Naye, Kamishna Msaidizi wa Jeshi la Magereza, Kizito Jacka alisema magereza yote hivi sasa yanakwenda kutumia nishati safi katika kupikia chakula cha wafungwa.

# Madiwani watwishwa zigo usimamizi ukusanyaji mapato

**Na Thobias Mwanakatwe,** MKALAMA

MADIWANI na wakuu wa idara katika Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama mkoani Singida wameagizwa kusimamia ukusanyaji wa mapato na kudhibiti mianya ya utoroshaji wa mazao, ili kuiwezesha halmashauri kufikia lengo la makusanyo katika mwaka fedha wa 2024/25.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama, James Mkwega aliyasema hayo juzi katika kikao cha baraza la madiwani cha robo ya pili cha kujadili utekelezaji wa shughuli za Serikali kwa kipindi cha Oktoba -Desemba kwa mwaka wa fedha 2023/24.

"Kila mmoja akitoka hapa akahakikishe anasimamia vyema suala la ukusanyaji wa mapato, diwani kwenye kata yako hakikisha unajua vyanzo vya mapato vilivyopo na kudhibiti utoroshwaji wa mazao kwani tayari msimu wa mazao umeanza ambayo ni chanzo kimojawapo cha mapato ya halmashauri," alisema.

Mwenyekiti huyo wa halmashauri pia aliagiza idara ya kilimo kutafuta namna ya kuhakikisha kuwa mashamba yote ya wakulima wilayani humo yanapimwa afya ya udongo kwa manufaa bora ya kilimo.

"Maisha yetu yanatokana na kilimo, kwahiyo maofisa ugani mkatumie hizo pikipiki mlizopewa kuwahudumia wananchi na siyo kuziweka ndani na kila robo tunapokutana hapa nataka taarifa ya maeneo yaliyofikiwa," alisema.

Diwani wa Kata ya Ibada, Salum Lindi alisema upimaji huo wa ardhi utawasaidia wakulima kujiingiza kwenye kilimo biashara ili kuongeza uzalishaji wa mazao mbalimbali na kujikomboa kiuchumi.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama, Abdalah Njelu alisema kuwa tatizo ni uhaba wa vitendea kazi na maofisa ugani na kwamba halmashauri itafanya jitihada kuhakikisha agizo la kupima afya ya udongo linatekelezwa.





# Wakulima, wafugaji Mbuyuni 'wazichapa' kisa malisho

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

MAPIGANO yameibuka kati ya wakulima na wafugaji katika Kijiji cha Mbuyuni kilichopo Kata ya Mapogoro Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya.

Wafugaji wa kijiji hicho wanadaiwa kuwacharaza bakora wakulima ambao walikamata mifugo hiyo, hali iliyowasababishia baadhi kuumia na wengine kuvunjika mikono.

Mmoja wa wakulima hao, Elia Chatila alisema wafugaji jamii ya wamaasai waliingiza mifugo shambani kwake na alipokwenda kuwazuia walimvamia na kumcharaza bakora.

Alisema kwa muda mrefu wamekuwa wakipata shida kutokana na makundi ya mifugo kuvamia mashamba yao na kula mazao hali ambayo inawatia hasara na hivyo kuendelea kuhatarisha hali ya amani na utulivu.

"Niliugulia mkono mpaka nikaenda kuponea katika Hospitali ya Ikonda iliyoko huko Makete, nilienda polisi na wakachukuliwa hatua lakini bado tatizo liko pale pale wanaendelea kuleta mifugo huku kwetu," alisema Chatila.

Winfrida Mbwilo alisema alikuwa amelima ekari mbili za alizeti na zilipofikia kimo cha kuanza kupalilia wafugaji waliingiza mifugo na kulishia mazao yote hali iliyomsababishia hasara kutokana na gharama alizotumia.

Alisema alipowakuta wafugaji hao alijaribu kuwazuia wakamtishia kwamba watampiga wamuumize ama kumuua kabisa hali iliyomfanya awaache na kuondoka kwenda kutoa taarifa kwa viongozi.

Alisema wafugaji hao walimwambia wako tayari walipe hata ng'ombe lakini wawe wameshamuumiza na hivyo akaiomba serikali kuingilia kati ili kumaliza tatizo hilo.

"Walinitisha sana nilikwenda kutoa taarifa kwa viongozi lakini mpaka sasa hakuna hatua yoyote ambayo imechukuliwa na hawa wafugaji bado wanaendelea kuchunga mifugo yao hapa," alisema Winfrida.

Naye Veronica Amiry alisema wafugaji hao walianza kuvamia maeneo yao Februari na kwamba mashamba mengi yameathirika na kuna hatari ya kukumbwa na baa la njaa.

Mwenyekiti wa chama cha wafugaji wa Kata ya Mapogoro, Kazi Mwakasala alikiri uwepo wa baadhi ya wafugaji ambao wanachunga kwenye mashamba ya wakulima na kwamba wamekuwa wakifanya jitihada mbalimbali kutatua migogoro hiyo.

Alisema serikali pia imekuwa ikifanya jitihada za kutatua migogoro hiyo ikiwemo kupanga matumizi bora ya ardhi lakini bado baadhi ya wafugaji wanaendelea kukiuka matumizi hayo kwa kuingia kwenye maeneo ambayo yametengwa kwa shughuli zingine.

"Wakulima wamekuwa wakija mara kwa mara kulalamika, kuna kipindi nilikaa na wafugaji na tukakubaliana kwamba hakuna mtu kuingiza mifugo kwenye mashamba ya wakulima, lakini bado tatizo lipo na tunaendelea kukabiliana nalo," alisema Mwakasala.



Mmoja wa wakulima wa Kijiji cha Mbuyuni, Kata ya Mapogoro, wilayani Mbarali mkoani Mbeya, akizungumza na waandishi wa habari juzi, kuhusu migogoro yao na wafugaji wanaodaiwa kuingiza mifugo kwenye mashamba. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Asilimia 3.5 ya mapato serikalini yanapotea kila siku

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

ASILIMIA 3.5 ya mapato ya serikali hupotea kila siku kutokana na wafanyabiashara kuuza bidhaa bila kutoa risiti ama kutoa risiti zenye viwango tofauti na uhalisia wa bei ya bidhaa wanazokuwa wameuza.

Ofisa Elimu na Mawasiliano wa Mamlaka ya Mapato nchini (TRA) Mkoa wa Mbeya, Aristariki Philipo aliyasema hayo juzi wakati maofisa wa mamlaka hiyo walipokuwa wanatoa elimu kwa wananchi kuhusu umuhimu wa kutoa na kudai risiti halali.

Alisema endapo wananchi wote watakuwa na utamaduni wa kudai risiti na wafanyabiashara wakawa wanatoa risiti halali, serikali ingekuwa inakusanya fedha za kutosha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo.

Alisema wananchi wanatakiwa kuchunguza risiti wanazopatiwa baada ya kununua bidhaa ili kujiridhisha kama fedha walizolipa ndizo zinazoandikwa kwenye risiti hizo kwa maelezo kuwa baadhi ya wafanyabiashara wamekuwa wakifanya udanganyifu.

Alisema wamekuwa wakifanya oparesheni ya kukagua risiti kwenye maeneo mbalimbali kwa ajili ya kuhakiki endapo wananchi wanadai risiti na kuchukua hatua mbalimbali kwa wale wanaokutwa na bidhaa ambazo wamenunua lakini hazina risiti.

"Ukishanunua bidhaa ukapatiwa risiti, hakikisha unakagua risiti husika ili kujiridhisha na kiwango cha fedha kilichoandikwa, ukinunua mzigo wa Sh. 100,000 halafu ukaandikiwa Sh. 50,000, tukikukamata lazima tukuchukulie hatua," alisema Aristariki.

Meneja wa TRA Mkoa wa Mbeya, Musibu Shabani alisema wameamua kuanza kutoa elimu kwa wananchi ili kuwaepusha na matatizo ya kutozwa faini ama kuchukuliwa hatua zingine za kisheria ambazo zinawaumiza zaidi.

Alisema watahakikisha wanatoa elimu katika maeneo yote ya mkoa huo ili elimu iwafikie wananchi wote na kuhakikisha kila mmoja anashiriki kuchangia mapato ya nchi.

Alisema wanapofanya ukaguzi hata kwenye magari wamekuwa wakikamata mizigo ambayo imenunuliwa lakini haina risiti ama ina risiti lakini kiwango cha fedha kilichoandikwa hakiendani na thamani halizi ya mizigo.

"Ukinunua dai risiti na ukiuza toa risiti, hapa kila mmoja atakuwa ameshiriki kuchangia maendeleo ya taifa letu, kwahiyo naomba kila mmoja atekeleze jukumu lake," alisema Shabani.

Baadhi ya wananchi walishauri maofisa wa TRA waendelee kutoa elimu hiyo kwa wananchi katika maeneo mbalimbali kwa maelezo kuwa elimu ya mlipakodi haijasambaa vya kutosha hasa maeneo ya vijijini.

Mmoja wa wananchi hao, Yusuph Jackson alisema kuna baadhi ya maduka huwa wakidai risiti wanapatiwa ambazo zinaandikwa kwa mkono na kusingizia kwamba mashine zina shida.

Alisema kuna uwezekano wakawa wanatumia mbinu hiyo kama sehemu ya kukwepa kodi na hivyo akawaomba maofisa hao kuendelea kutoa elimu.

## Tatizo wanafunzi Iganzo kukaa chini lapatiwa ufumbuzi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

TATIZO la wanafunzi wa Shule ya Msingi Juhudi iliyopo Kata ya Iganzo katika Halmashauri ya Jiji la Mbeya kukaa chini na baadhi kubanana kwenye madawati limepungua baada ya serikali kuanza kupeleka samani hizo.

Mwalimu Mkuu wa Shule hiyo, Josephat Mwaigaga alisema shule ina wanafunzi 2,414 na kwamba ilikuwa na upungufu wa madawati 244 hali iliyokuwa inasababisha baadhi ya wanafunzi kukaa chini na wengine kukaa zaidi ya wawili kwenye madawati machache.

Alisema kwa sasa serikali imeshapeleka madawati 100 na sasa wamebakiwa na upungufu wa madawati 144 na wameahidiwa na serikali kwamba yanatengenezwa yakiwa tayari yatapelekwa.

Alisema kitendo cha wanafunzi kukaa chini ama kubanana kwenye madawati kinasababisha hata ufaulu wa wanafunzi kushuka na baadhi kutopenda kwenda shule.

"Tunaishukuru Serikali imetusaidia kwa haya madawati na bahati nzuri mkurugenzi ametuahidi kwamba mengine wanayakamilisha na watatuletea, tunaamini hili tatizo linakwenda kuisha kabisa," alisema Mwalimu Mwaigaga.

Alisema shule hiyo ina idadi ya kutosha ya vyumba vya madarasa lakini baadhi havina madawati na kwamba wanakusudia hayo yatakayopelekwa yatawekwa kwenye vyumba hivyo.

Mkurugenzi wa Jiji hilo, John Nchimbi alisema halmashauri hiyo imepanga kutengeneza madawati zaidi ya 6,000 na kuyasambaza kwenye shule mbalimbali ambazo zina upungufu na kwamba idadi hiyo ya madawati ndiyo yalikuwa yanahitajika. Alisema waligawa tenda ya kutengeneza madawati hayo ambapo baadhi yanatengenezwa na Chuo cha Ufundi Stadi (VETA) na baadhi yanatengenezwa na mafundi wa mtaani.

Hivyo, aliwataka walimu na kamati za shule kuhakikisha wanatunza vifaa vyote ambavyo vinasambazwa shuleni ili vidumu na kuwasaidia wanafunzi kwa muda mrefu.



# TAMWA yakumbusha wazazi kulinda watoto sikukuu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

CHAMA cha Wanahabari Wanawake Tanzania (TAMWA), Zanzibar kimewataka wazazi na walezi kuendelea kuwalinda na kuhakikisha usalama wa watoto wao hasa katika kipindi hiki cha sherehe za Sikukuu za Eid el Fitr.

Akitoa taarifa kwa vyombo vya habari jana, Mkurugenzi wa TAMWA Zanzibar, Dk. Mzuri Issa, alisema chama hicho kinaungana na jamii katika sherehe hizo, lakini lazima jamii ikimbuke majukumu ya kulinda usalama wa watoto.

Alisema uzoefu unaonesha kipindi cha sikukuu wahalifu hutumia mwanya kwa kuwadhalilisha watoto kwa sababu wanakuwa huru muda mwingi kusherehehekea sikukuu.

"Hivi karibuni tumeendelea kushuhudia ongezeko la matukio ya udhalilishaji, kutoka matukio 1,360 mwaka 2022 hadi 1954 mwaka 2023, ambapo ni sawa na ongezeko la asilimia 43.7, hii ni kwa mujibu wa ripoti ya Mtakwimu Mkuu ambayo pia inaonesha kuwa waathirika wengi wa matukio haya ni watoto na kwa mwaka 2023 walikua asilimia 83.7 ya waathirika wote," alisema Dk. Mzuri.

Alisema lazima wazazi na walezi waongeze jitihada kupunguza matukio hayo kwa kuwa karibu na watoto wao na kuzifuatilia nyenendo za watoto kwa kipindi chote.

"Tunatambua pia umuhimu wa kulinda na kudumisha maadili hasa katika upande wa mavazi na mienendo kwa lengo la kuhakikisha usalama wa watoto wetu. Kipindi hiki cha sikukuu ni fursa ya kipekee ya kuzingatia maadili haya na kuiweka jamii yetu katika mstari unaofaa," alisema.

Aidha, Jeshi la Polisi visiwani humo limesema litaendelea kuimarisha ulinzi na usalama wa raia na mali zao katika kipindi chote hasa cha sikukuu.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kusini Unguja, Daniel Shila, alisema jeshi hilo litaimarisha ulinzi katika maeneo ya nyumba za ibada, viwanja na kumbi za starehe, pamoja na kusimamia vyema Sheria za Usalama Barabarani.

Aliwataka wananchi kuhakikisha katika nyumba zao anabaki mtu japo mmoja ili kutotoa mwanya kwa wahalifu kufanya vitendo vya wizi.

Naye Kaimu Kamanda wa Mkoa wa Mjini Magharib Unguja, Abubakar Khamis Ally, alisema kutokana na umuhimu mkubwa wa sikukuu hiyo, jeshi hilo limejipanga vyema kuimarisha ulinzi na usalama katika maeneo yote ikiwamo viwanja vya sikukuu, kuimarisha usalama barabarani, doria na misako mitaani na maeneo mengine ili isherehekewa kwa amani utulivu.

Akizungumzia muda wa kufunguliwa na kufungwa viwanja vya sikukuu aliwataka wananchi kufuata sheria na taratibu za muda huo ikiwamo viwanja kufungwa saa 4:00 usiku ili kuepusha usumbufu pamoja na vitendo vya kihalifu.

Kaimu Abubakar aliwasisitiza wamiliki wa kumbi za starehe na wamiliki wa baa ifikapo saa 6:00 kamili usiku zinafungwa, isipokuwa kwa wenye leseni za kufanyakazi usiku.

Aidha, kwa upande wa usalama barabarani, alisema baadhi ya barabara zitafungwa kwa muda kwa kipindi chote cha sikukuu na askari wa watakua katika barabara mbalimbali ili kudhibiti madereva wazembe na wasiotaka kutii sheria za usalama barabarani.

Aliwaomba madereva wa vyombo vya moto ikiwamo magari, pikipiki, bajaji na vyombo vingine vya usafiri kuwa na tahadhari wanapoendesha vyombo hivyo kwa kuzingatia sheria ili kuepusha ajali.

# Wajasiriamali wahamasishwa kupikia gesi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais Uchumi na Uwekezaji, Sharifu Ali Sharifu, amewataka wajasiriamali kuacha kutumia nishati ya gesi ili kuhifadhi mazingira.

Akizungumza jana katika hafla ya kukabidhi majiko ya gesi kwa wajasiriamali na wananchi wa Mkoa wa Mjini yaliyotolewa na kampuni ya Oryx Gas kwa kushirikiana na Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Tabia Mauli Mwita, alisema wajasiriamali wanawake ndio watumiaji wakubwa wa nishati ya kuni na mkaa kupikia na kuwataka kubadilika kutumia gesi ili kurahisisha shughuli zao na kupunguza matumizi ya kuni na mkaa.

Waziri Tabia alimpongeza Rais wa Jamhuri ya Muumgano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan kwa kuwawezesha wajasiriamali na makundi mbalimbali kuanzisha kampeni matumizi ya nishati ya gasi kwa kuleta mradi huo wa majiko ya gesi ili kudhibiti ukataji wa misitu na kuhifadhi mazingira.

Meneja Mkuu wa Oryx Gas Zanzibar, Shuwekha Khamis Juma, alisema kampuni yao inaamini iwapo wananchi wakitumia gesi kwa kupikia inaleta maendeleo makubwa nchini.

Alisema matumizi ya gesi yanalinda mazingira kutokana na kutokomeza ukataji wa miti kwa ajili ya kutengeneza mkaa na kuni na misitu ni muhimu kwa kudumisha viumbe hai, kuhifadhi udongo, kusaidia mzunguko wa maji na uharibifu wa misitu inaharibu mifumo ya ekolojia na rasilimali za asili.

Pia, matumizi ya nishati ya gesi ya kupikia yanasaidia kulinda afya ya wanawake ambao wanaathirika kwa moshi unaotokana na mkaa na kuni na kuwaepusha mama na watoto kuumia kwa kubeba mizigo mizito ya kuni.

Alisema matumizi ya nishati ya gesi kwa wanawake yanasaidia kufanya shughuli mbalimbali ikiwamo ya ujenzi wa taifa kutokana na kupika kwa haraka bila kuharibu ubora na ladha ya chakula.

Alisema kampuni ya Oryx Gas itaendelea kuunga mkono ajenda ya Rais Samia ya kuhimizi kutumia gesi katika shughuli mbalimbali ili kuleta maendeleo katika nchi na kuboresha maisha ya wananchi. Waziri Tabia alisema lengo la kutoa majiko hayo kwa wajasiriamali wadogo ni kuunga mkono juhudi zao na kuwawezesha kutumia nishati sahihi kwa ajili kazi zao.

Mbunge wa Viti maalumu Mkoa wa Mjini Unguja, Asha Abdalla Juma, aliipongeza Kampuni ya Oryx gas kwa kumuunga mkono Rais na kuwawezesha wajasiriamali wanawake kupata nishati ya kupikia.

Jumla ya mitungi ya gesi 200 ya kilo sita imetolewa kwa wananchi na wajasiriamali mkoani humo ili kukabiliana na athari za kimazingira zitokanazo na matumizi ya nishati ya kuni na mkaa.




Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji Zanzibar, Sharif Ali Sharif (katikati) na Meneja Mkuu wa kampuni ya Oryx Gas Zanzibar, Shuwekha Khamis (kushoto), wakimkabidhi jiko la gesi kwa mjasiriamali Ngaza Khamis mkaazi wa Kwahani, mjini Unguja, wakati wa hafla ya ugawaji wa majiko kwa wajasiriamali wa wilaya ya mjini juzi katika. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Kamati Baraza Wawakilishi yaridhishwa ripoti ya ZICTIA

**Na Mwandishi Wetu**

KAMATI ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali ya Baraza la Wawakilishi imesema imeridhishwa na uwasilishwaji wa ripoti ya Taasisi ya Mawasiliano Zanzibar (ZICTIA).

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Juma Ali Khatib, aliyasema hayo katika kikao hicho kilichofanyika Unguja, juzi.

Baada ya kupokea ripoti hiyo Juma alisema ameridhika pamoja na ushirikiano mkubwa walioupata kupitia hoja za Mdhibiti Mkuu wa Serikali kuhusu ukaguzi wa fedha za Mashirika na Taasisi zinazojitegemea za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kipindi cha mwaka wa fedha unaoishia Juni 30.

Alisema Kamati ya PAC inaishauri kuongeza ufanisi katika kuandaa taarifa za fedha za mwaka ili zisitokee dosari zozote katika hesabu za fedha za serikali.

Naye Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Dk. Khalid Salum Mohamed, aliishukuru kamati hiyo kwa kutoa ushirikiano, ushauri pamoja na miongozo walioitoa na kuahidi watayafanyia kazi kikamilifu.

# Magereza, REA waingia mkataba wa bilioni 35/- nishati safi

**Na Renatha Msungu** DODOMA

JESHI la Magereza nchini limetia saini mkataba wenye thamani ya Sh. bilioni 34.9 na wakala wa Nishati Vijijini (REA) wa matumizi ya nishati safi katika Magereza 129 nchini ili kuepuka uchafuzi wa mazingira na athari kwa binadamu zitokanazo na moshi wa kuni.

Akizungumza wakati wa utiaji saini mjini Dodoma, Mkuu wa Jeshi la Magereza, Kamishna Jenerali Ramadhan Nyamka, alisema jeshi hilo linaachana na matumizi ya kuni na kutumia nishati safi kwa kupika vyakula vya Magereza.

"Tunawashukuru sana REA kwa kuingia mkataba nasi niwahakikishie nishati safi itaendelea kutumika katika Magereza yetu mbalimbali hapa nchini," alisema Kamishna Jenerali Nyanja.

Pia, wanaishukuru kwa kutoa baadhi ya majiko kwa askari kama moja ya kushawishi askari wengine kutumia nishati hiyo.

Aidha, nishati safi itarahisisha maandalizi ya vyakula vya Magereza na kutumia muda mfupi.

Mkurugenzi wa REA, Hassan Said, alisema wataendelea kutoa ushirikiano kwa jeshi hilo ili kupata watu wanaojua kunitumia nishati hiyo.

Alisema walianza mchakato wa miezi sita kwa ajili ya matumizi ya nishati safi, wanashukuru Magereza wamekuwa wa kwanza kutumia nishati hiyo.

Vile vile, alisisitiza wengine wajitokeze kutumia nishati hiyo kwa ajili ya matumizi ya nyumbani na taasisi pia.

Kamishna Msaidizi wa Jeshi la Magereza, Kizito Jacka, alisema Magereza zote zinahamia kwenye matumizi ya nishati safi kwa kupikia chakula cha wafungwa.

Serikali ilitoa tamko kuanzia Januari Mosi, mwaka huu taasisi zianze kutumia nishati safi kwa kupikia.



Bharat Nathwan (kushoto), akitoka katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam juzi, kusikiliza kesi inayomkabili ambapo anatuhumiwa kosa la kumjeruhi jirani yake, Lalit Kanabar. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Serikali yaombwa kukamilisha miradi iliyoanzishwa kwa nguvu za wananchi

**Na Zanura Mollel**

BAADHI ya wakazi wa Dar es Salaam wameomba serikali kukamilisha miradi iliyoibuliwa na kujengwa kwa nguvu za wananchi baada ya kutenga fedha za uanzishwaji wa miradi mipya katika maeneo yao.

Akizungumza katika mdahalo ulioandaliwa na Mtandao wa Jinsia (TGNP) Mabibo, jijini Dar es Salaam, mwezeshaji Deogratius Kayango alisema, maeneo mengi wananchi wameanza ujenzi wa majengo ya afya na elimu yakiwa yamefikia hatua ya lenta.

Alisema ni vyema wananchi wakawa mstari wa mbele kuwauliza viongozi wao wakati sahihi wa kuwasilisha maoni kuhusu mchakato wa maandalizi ya bajeti ya mwaka wa fedha unaotarajiwa.

"Wananchi wasipopeleka vipaumbele vyao kwenye maandalizi ya bajeti, Inawapa nafasi Ofisa mipango au serikali ya mtaa kuibua miradi ambayo sio kipaumbele kwao," alisema Deogratius.

Alisema kila mwananchi ana mchango mkubwa wa kulipa deni la taifa ikiwa ni pamoja na ushuru kwa kununua bidhaa mbalimbali pamoja na kulipa kodi kwa shughuli za kibiashara wanazotekeleza.

Alifafanua kuwa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977 inaeleza kuwa mamlaka yote ya serikali na viongozi inatoka kwa wananchi, nao wana haki ya kushiriki katika mchakato wa uandaaji wa bajeti na utekelezaji wake (matumizi).

Akielezea umuhimu wa mamlaka za serikali za mitaa, alisema ibara ya 145 na 146 kwenye Katiba inaeleza serikali hiyo ni vyombo vya haki vyenye mamlaka ya kushiriki na kushirikisha katika kupanga na kutekeleza shughuli za maendeleo na utoaji wa huduma katika sehemu zao.

"Serikali za mitaa zimeanzishwa kwa madhumuni ya kuwahudumia wananchi na kuwapelekea madaraka kwa kuwajengea uwezo wa kiuchumi, kijamii, kisiasa na kitamaduni," alisema Deogratius.

Lucy Mwanasanga, mkazi wa Mabibo alisema changamoto kubwa inayochangia wananchi katika maeneo yao kutoshiriki mkutano mkuu wa serikali ya kijiji na mchakato wa maandalizi ya bajeti ni hali ngumu ya maisha. "Wananchi wakiambiwa kuna mkutano wanauliza kama kuna malipo, huku wakiwa na msimamo wa madai kama hakuna pesa hawapo tayari kushiriki katika mkutano."

"Hata wakati wa kupiga kura hali ni hiyo hiyo hawajitokezi mambo yakiwa magumu wanalalamika," alisema Mwanasanga.

Tatu Kitenjo, alisema mfumo wa chama kimoja katika uongozi umechangia kuwanyima fursa wananchi kuwasilisha mawazo yao katika uandaaji wa bajeti na shughuli za maendeleo kwenye maeneo yao.

Aidha, Elizabeth Kiteleka alisema baadhi ya viongozi kutokutambua wajibu wao kwa jamii na kutoitisha vikao vya kisheria kumesababisha wananchi kushindwa kuchangia katika maandalizi ya bajeti ya mwaka wa fedha 2024/25.

# Mashindano ya mikoa kuvutia uwekezaji kuanza

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Prof. Kitila Mkumbo, amesema katika kuchochea uwekezaji na biashara nchini kwenye mikoa na halmashauri, itaanzisha mashindano yatakayoonesha uvutiaji uwekezaji.

Akizungumza jana kwenye mafunzo ya Makatibu Tawala wa mikoa na Wakurugenzi wa halmashauri jijini hapa, Prof. Mkumbo alisema lengo ni kuhamasisha ubunifu na mbinu za kuongeza uwekezaji na biashara kwenye maeneo yao.

"Tunataka tuone mnavyovutia uwekezaji, tutatengeneza vigezo na tutapimana kwa mujibu wa hivyo vigezo kama uwekezaji hautokei hakuna uchumi mpya, tunataka kuona mnachochea vipi uwekezaji maana miundombinu inajengwa SGR (reli ya kisasa) inajengwa kusafirisha mizigo bila biashara itafanya kazi gani. Tutawaona wanaofanya vizuri na vibaya katika kuwezesha biashara na mazingira ya uwekezaji," alisema.



Aidha, aliwataka viongozi hao kushiriki kuwezesha ufanyaji biashara kwenye maeneo yao ili kukusanya kodi bila kukwamisha wananchi au kuwakandamizi.

"Kuna changamoto katika serikali katika suala la biashara wengi wamejikuta wakidhibiti na sio kuwezesha, walipakodi namba moja ni wafanyabiashara ili tupate mishahara yetu ni lazima kodi zilipwe, ili kodi zilipwe lazima biashara zifanyike, lazima tuweke mazingira ya kufanya biashara," alisema.

Alisema katika maeneo mengi wafanyabiashara wanapokaguliwa leseni wanachofanyiwa ni kudhibitiwa mfano kulazimishwa kufunga biashara jambo ambalo sio uwezeshaji wa biashara.

"Msichangie kukwamisha biashara inahatarisha usalama wa nchi kwani ikitokea watumishi wa umma wanakuwa hawana utulivu basi serikali haiwezi kuwa na utulivu, ukikwamisha biashara unakwamisha kodi," alisema.

## HABARI KIMATAIFA/KITAIFA

# Zuma aruhusiwa kushiriki uchaguzi

**PRETORIA,** Afrika Kusini

RAIS wa zamani wa Afrika Kusini Jacob Zuma, hatimaye atashiriki katika uchaguzi mkuu uliopangwa kufanyika mwishoni mwa mwezi Mei.

Kiongozi huyo mwenye ushawishi nchini humo, alizuiwa mwezi uliopita na Tume ya Uchaguzi (IEC) kushiriki katika uchaguzi huo.

Hata hivyo, chama chake kipya kilichukua hatua za kisheria wiki iliyopita ili kutaka uamuzi huu ubatilishwe na kukubaliwa jana.

Rufani hiyo ilikubaliwa na mahakama ya uchaguzi katika uamuzi ambao shirika la habari la AFP limepata kopi yake.

Jacob Zuma ni mgombea katika orodha ya chama kipya chenye siasa kali kilichoundwa hivi karibuni kinachoitwa Umkhonto We Sizwe (MK) ikimaanisha mkuki wa taifa kwa lugha ya Kizulu.



Zuma ambaye alikuwa nguzo ya chama cha African National Congress (ANC) ambacho kipo madarakani kwa miaka 30, aliibua mshangao kwa kutangaza kukiunga mkono chama cha MK katika uchaguzi mkuu.

Tangu kuanza kwa kampeni, mvutano umekuwa ukiongezeka kati ya ANC na MK. Ambapo mwezi Machi, mahakama ilikataa ombi la chama tawala kutaka MK iondolewe kwenye orodha ya vyama vilivyosajiliwa kwa ajili ya kushiriki uchaguzi huo.

Uamuzi bado unasubiriwa baada ya ANC kuwasilisha rufaa nyingine. **RFI**

## Tume ya uchaguzi yabadilishwa jina rasmi

**Na Romana Mallya**

IDARA ya Habari-MAELEZO, imetangaza kuhusu mabadiliko ya jina la Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) ambayo kwa sasa itatambulika kama Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC).

Mkurugenzi wa Idara ya Habari na Msemaji Mkuu wa Serikali, Mobhare Matinyi, kupitia taarifa yake kwa vyombo vya habari jana, alisema mabadiliko hayo yataanza kesho jina la tume hiyo litatambulika hivyo.

"Tunapenda kuvitaarifu vyombo vyote vya habari kwamba kutokana na tangazo la Serikali Na. 225 la Machi 29, 2024, Sheria ya Tume Huru ya Huru ya Taifa ya Uchaguzi Na. 2 ya mwaka 2024, itaanza kutumika rasmi Aprili 12, 2024," alisema.

Alisema kuanzia sasa jina la tume hiyo litatambulika hivyo kwa lugha ya Kiingereza itakuwa Independent National Electoral Commission (INEC).

Novemba 10, 2023, miswada mitatu ya sheria za uchaguzi ilisomwa kwa mara ya kwanza bungeni na kuanza kujadiliwa katika Mkutano wa 14 wa Bunge la 12 ulioanza Januari 30 hadi Februari 16, 2024.

Miswada hiyo ilikuwa ya Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani wa Mwaka 2023 na Sheria ya Tume ya Uchaguzi wa Mwaka 2023.

Miswada mingine ni Sheria za Vyama vya Siasa wa Mwaka 2023 na Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2023.

Aprili 3, mwaka huu, Spika Dk. Tulia Ackson, aliujulisha umma kupitia bunge kuwa Rais Samia alishatia saini miswada hiyo kuwa sheria kamili na tayari imeshatangazwa kwenye gazeti la serikali.



Hali inazidi kuwa mbaya nchini Haiti, pichani ni baadhi ya polisi wachache wanaolinda baadhi ya maeneo ya mji mkuu. **PICHA: AP**

## Mawakili vitani kusaka vishoka wa mihuri yao

**Na Restuta James**

WAKILI Aristarko Msongela ametoa angalizo la kushamiri vishoka wa kazi hiyo na kupendekeza Chama cha Mawakili Tanganyika (TLS) kiwe na mwendesha mashtaka binafsi wa kusimamia kesi za 'makanjanja' wa sheria.

Katika hilo, Rais wa TLS, Harold Sungusia, ameonya kuwa kosa la mtu kujifanya wakili (kishoka). Faini ni kati ya Sh. milioni tano hadi milioni 20, kifungo cha mwaka mmoja hadi mitatu au vyote kwa pamoja.

Barua ya Wakili Msongela kwa Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa TLS, aliyoiandika juzi na Nipashe kuona nakala yake jana, inaeleza kuwa mbali ya mwendesha mashtaka binafsi, mihuri mipya ya kieleketroniki inayotumiwa na mawakili, iwe na neno siri ambalo litaizuia kutumika bila idhini ya wakili husika.

"Mihuri mipya iweze kufuatiliwa na mfumo na ukitia saini nyaraka yoyote, taarifa ije kwa wakili kwa njia ya simu kuwa mhuri fulani umetumika kusaini nyaraka... nyaraka zikipokewa wakili apate ujumbe," anasema.

Anapendekeza kuwapo kamati ya kukabili vishoka (Anti-vishoka taskforce committee); iwe ni kamati rasmi ya kudumu na itajwe katika sheria, iwe huru na iripoti kwa TLS na iwe na polisi wa kike na wa kiume watakaofanya nayo kazi.

Anasema vita dhidi ya vishoka imekuwa ngumu kutokana na mtandao wao kuwa mkubwa na baadhi ni madalali wa kuunganishia mawakili kazi.

Wakili huyo anasema asilimia 70 ya vishoka wanatengenezwa na mawakili wenyewe kwa kuajiri watu wasio na sifa za uwakili, jambo linalowafanya watumie ofisi vibaya wanapoondoka.

"Kwa asilimia 10, taasisi mbalimbali na watu binafsi wasiotakia mema taaluma ya uwakili, mfano zipo zinazofanya kazi na baadhi ya mawakili na kupanga bei ambazo ni kiwango kidogo sana na asilimia tano ni sisi mawakili tunaiharibu kwa kuajiri wapigadebe na kugawana nao mapato," anasema.

Wakili huyo anasema maduka yanayouza vifaa vya shule yanazalisha vishoka kwa asilimia 15 kwa kuwa yanahudumia wananchi wengi kwa wakati mmoja na yanakuwa na mihuri ya mawakili.

"Kwa sasa kuna tishio kubwa kwa mihuri hii inayoitwa ya kielektroniki kwani tayari baadhi ya vishoka wameanza kufanya nukushi, kugushi na kutia saini nyaraka mtandaoni na kuzituma katika taasisi mbalimbali. Bahati mbaya hakuna namna ya kutambua mhuri wa wakili fulani umetumika," anasema.

Katika ufafanuzi wake kwa mwandishi jana jioni, Sungusia alisema wigo wa vishoka ni mkubwa; mwaka jana Bunge lilifanya marekebisho ya sheria mbalimbali na kuongeza adhabu kwa vishoka.

"Kupitia Sheria Na. 11 ya 2023 ambayo Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alitia saini Novemba 19, 2023 na ikaanza kutumika Desemba Mosi, 2023, ilirekebisha kifungu cha 41 na 42 ya Sheria ya Mawakili kwa lengo la kuongeza adhabu kwa vishoka kutoka Sh. milioni moja au kifungo cha mwaka mmoja na kufanya adhabu ya vishoka sasa kuwa faini kati ya Sh. milioni tano hadi Sh. milioni 20 au kifungo kati ya mwaka mmoja hadi mitatu au vyote viwili - faini na kifungo," alisema.

Kuhusu kuendesha mashtaka binafsi kwa vishoka, Sungusia alisema ni ombi la TLS kwa vyombo vya dola, kwa kuwa chama hicho kina uwezo wa kufanya kazi hiyo.

"Hata hivyo, Sheria ya Huduma za Mashtaka Sura Na. 430 inampa madaraka Mkurugenzi wa Mashtaka kusimamia mashtaka yote. Utaratibu wa mashtaka binafsi unaruhusiwa na sheria lakini mwenye madaraka ya kikatiba kuhusiana na mashtaka ya jinai nchini ni DPP (Mkurugenzi wa Mashtaka).

"TLS bado inafuatilia uwezekano wa kupata kibali cha kuendesha mashtaka dhidi ya vishoka maana uwezo huo tunao na italeta heshima kwa kada ya mawakili na kuhakikisha raia hawaumizwi na ulaghai wa vishoka," alisema.

Alisema malalamiko ya wakili Msongela yameainisha namna ambavyo uhalifu unaendelea kutanuka na kwamba kazi ya TLS ni kuendelea kuimarisha mifuko ya kudhibiti uhalifu kwa kadri inavyowezekana.

"Kamati yetu ya TLS ya Maadili ya Mawakili imekuwa inafanya kazi kubwa sana kuhakikisha tunadumisha heshima na hadhi ya mawakili nchini," alisema Wakili Sungusia.

# LIGI YA MABINGWA AFRIKA YAIBEBA PRISONS LIGI KUU

Na Adam Fungamwango

TIMU ya Prisons imesema mapumziko ya kupisha mechi za mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika iliyochezwa kwa wiki mbili nyumbani na ugenini, pamoja na Kalenda ya FIFA, imewasaidia kukisuka upya kikosi chao na sasa wanaamini 'kitakuwa moto' katika michezo ya lala salama.

Kocha Mkuu wa Prisons, Ahmad Ally, aliliambia gazeti hili wakati Simba na Yanga wakiiwakilisha Tanzania katika michuano hiyo ya kimataifa, michezo ya Ligi Kuu Bara ilisimama na alitumia muda huo kurekebisha mapungufu yote yaliyojitokeza katika kikosi chake.

**Hamad alisema pia muda huo wa mapumziko uliwasaidia wachezaji wake waliokuwa na uchovu kupumzika na anaamini watarejea na nguvu mpya katika michezo inayofuata.**

"Kusema kweli Ligi ya Mabingwa Afrika imetubeba sana, imetubeba vipi? Ni kwa sababu wakati timu za Tanzania zinacheza kulikuwa na mapumziko ambayo sisi kama Prisons tumeyatumia vizuri. Kwa sababu wakati ligi inachezwa kunakuwa hakuna muda wa kufanya masahihisho, badala yake mechi zinakuwa mfululizo pamoja na safari," alisema kocha huyo.

Aliongeza muda wote huo yeye alikuwa anafanya kazi kwa vitendo na aliendelea na mazoezi akilenga zaidi kufanyia kazi mapungufu ambayo ameyaona katika kila idara.

"Tumeangalia mapungufu kuanzia golini hadi kwenye ushambuliaji, nadhani sasa tunaweza tukawa vizuri sana kuliko hata mwanzo, kama mimi mwalimu nashukuru sana michuano hiyo kwa sababu imetusaidia kupata muda mwingine kuandaa kikosi, na hii ni wiki ya mwisho kuelekea katika michezo yetu, hasa huu kwanza unaofuata dhidi ya KMC," Hamad alisema.

Prisons itajitupa kwenye Uwanja wa nyumbani wa CCM Sokoine kucheza dhidi ya KMC, ikiwa ni mechi ya raundi ya 22 ya Ligi Kuu Tanzania Bara, na baada ya hapo itakuwa imebakisha michezo nane tu ili kumalizia msimu.

Katika msimamo wa ligi, Maafande hao wako kwenye nafasi ya tano wakiwa na pointi 28, na ni moja kati ya timu zinazowania moja kati ya nafasi nne za juu kwa ajili ya kuiwakilisha Tanzania Bara katika michuano ya kimataifa msimu ujao.

Yanga ndio vinara na mabingwa watetezi wa ligi hiyo inayoshirikisha timu 16 kutoka mikoa mbalimbali ya Tanzania Bara.



Washiriki wa kozi ya Grassroot kutoka miji ya Loliondo na Ngorongoro, Arusha wakiwa katika picha ya pamoja baada ya kumaliza mafunzo ya siku tano. **PICHA: TFF**

# Uzio mpya wajengwa CCM Sokoine

Na Adam Fungamwango

UWANJA wa CCM Sokoine wa jijini, Mbeya umeanza kufanyiwa ukarabati huku kwa mara ya kwanza ukiwekwa uzio mpya mrefu kwa ajili ya kuzuia mashabiki wakorofi kuingia katika eneo la kuchezea, imeelezwa.

Uwanja huo unakarabatiwa na Chama cha Mapinduzi (CCM) mkoani humo, ambapo katika ukarabati wake unajumuisha maeneo mbalimbali muhimu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Meneja na Msimamizi wa uwanja huo, Modestus Mwaluka, alisema ukarabati unafanyika unalenga kuuboresha uwanja huo mkongwe ili kuupandisha kiwango chake.

"Awamu ya kwanza tumeweka nyavu kuzunguka uwanja, hili ndilo lilikuwa la kwanza, wenzetu wa TFF (Shirikisho la Mpira wa Miguu Nchini (TFF), walikuwa wanatupigia kelele sana kuwa uzio wa nyavu tulioweka ni mfupi sana kwa kwenda juu na kusababisha mashabiki kuruka na kuingia ndani baada ya mechi, sasa tumeweka hizi mpya ndefu, hakuna mtu anaweza kuingia uwanjani kirahisi," alisema meneja huyo.

Aliongeza awamu ya pili ambayo imeshaa kwa sasa ni kupaka rangi uwanja mzima, huku tayari jukwaa kuu likiwa limeshapakwa.

"Awamu ya pili tunayokwenda nayo ni kupaka rangi uwanja mzima, tumeanza na jukwaa kuu na juu ya bati kuna sehemu ndogo inavuja, kwa hiyo ni lazima baadhi ya mabati tuyatoe na kuweka mengine. Kuna watu wanaoonyesha na kurekodi mipira, tunawawekea ngazi mpya ili wapande vizuri juu wasije kuanguka na kamera zao," alisema Mwaluka.

# Mgosi aanika siri mechi za kirafiki

Na Saada Akida

KOCHA Msaidizi wa Simba Queens, Mussa Hassan 'Mgosi', amesema mechi za kirafiki walizocheza zimesaidia kukiweka imara kikosi chake ili kuwa tayari kukabiliana na ushindani wa michezo ya mzunguko wa pili wa Ligi Kuu ya Soka ya Wanawake Tanzania.

Simba Queens itaanza mzunguko wa pili kwa kuifuata Ceasea mechi itakayochezwa Aprili 15, mwaka huu kwenye Uwanja wa Samora, Iringa.

Simba Queens ilicheza mechi tatu za kirafiki mbili dhidi ya Kinondoni Queens na moja dhidi ya Serengeti Girls, mechi zote waliibuka na ushindi.

Akizungumza na Nipashe jana, Mgosi alisema katika mechi hizo hawakua na malengo pekee ya kushinda, lakini walihitaji kuangalia utimamu wa mwili wa wachezaji baada ya kukaa muda mrefu bila ya kucheza michezo ya ushindani.

Mgosi alisema kulingana na maandalizi waliyoyafanya anaamini wakiwa ugenini Iringa kuwafuata Ceasiaa Queens watapambana kuondoka na pointi tatu.

"Maandalizi yanaendelea vizuri kama tulivyoesma awali, malengo yetu ya msimu huu ni kurejesha heshima ya Simba, kutwaa ubingwa, kufikia hapo lazima tufanye vizuri na kusaka ushindi katika michezo iliyopo mbele yetu," alisema Mgosi.

Aliongeza wanahitaji kuendelea kutafuta matokeo chanya katika kila mechi ili kujiweka kwenye mazingira mazuri ya safari yao ya kuwania taji la Ligi Kuu ya Soka ya Wanawake Tanzania.

Alisema vinara hao wa ligi hiyo ya wanawake wataondoka Dar es Salaam kesho ili kuelekea Iringa tayari kwa mchezo huo wa duru la pili.

Mechi nyingine za ligi hiyo zitakazochezwa Aprili 15, mwaka huu ni kati ya mabingwa watetezi, JKT Queens dhidi ya Bunda Queens, uwanja wa Mej General Isamahyo huku Geita Gold Queens watawakaribisha Alliance Girls kwenye uwanja wa Shule ya Sekondari Nyakumbu.

Mchezo mwingine utakuwa kati ya Amani Queens dhidi ya Fountain Gate FC katika dimba la Ilulu, Lindi na Yanga Princess watakuwa nyumbani dhidi ya Baobab Queens, uwanja wa Azam Complex uliopo, Dar es Salaam.



Simba Queens wakiwa mazoezini. **PICHA: MAKTABA**

## ZISIKUPITE

### WILLIAMS ATAKIWA SPURS

KLABU ya Tottenham Hotspur inamfuatilia mshambuliaji wa Athletic Bilbao mwenye umri wa miaka 21, Nico Williams, ambaye ana kipengele cha kuachiliwa kwa pauni milioni 42.8 katika mkataba wake. ***(Sport)***

### JOELINTON KUTUA NEWCASTLE

MAZUNGUMZO kati ya Newcastle United na kiungo wa kati wa Brazil, Joelinton, yanaendelea vyema na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 anakaribia kusaini mkataba mpya na klabu hiyo ya Tyneside. ***(Telegraph)***

### VARANE, CASEMIRO KUUZWA

MLINZI Mfaransa, Raphael Varane, mwenye umri wa miaka 30, na kiungo wa kati wa Brazil, Casemiro (32), wanatarajiwa kuongoza orodha ya wachezaji ambao Manchester United itawauza msimu wa joto. ***(Talksport)***

### LIVER KUMWACHIA SALAH

LIVERPOOL ipo tayari kumruhusu Mohamed Salah kuhamia Ligi Kuu ya Saudi Arabia maarufu kama Saudi Pro League mwishoni mwa msimu huu, ikiwa fowadi huyo wa Misri mwenye umri wa miaka 31 ataweka wazi anataka kuondoka. ***(HITC)***

### CITY YAMWANIA NETO

KLABU ya Manchester City inavutiwa na winga wa Wolves, Pedro Neto lakini huenda wakakabiliana na ushindani kutoka kwa klabu za Saudi Arabia kumnunua mchezaji huyo wa kimataifa wa Ureno mwenye umri wa miaka 24. ***(Teamtalk)***

### PALACE, FULHAM VITANI

KLABU za Crystal Palace na Fulham zinalenga kumnunua mlinzi wa Union Berlin ya Uholanzi, Danilho Doekhi, mwenye umri wa miaka 25. ***(Football Insider)***

### RODRYGO ALIIKATAA LIVER

MSHAMBULIAJI wa Real Madrid, Rodrygo, mwenye umri wa miaka 23, amesema alikataa kuhamia Liverpool mwaka wa 2017, ingawa Wekundu hao walikuwa na ofa ya euro milioni tatu kwa mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil iliyokubaliwa na Santos. ***(O Dia)***

### FRIMPING ANUKIA LIVERPOOL

MLINZI wa pembeni wa kulia wa Bayer Leverkusen ambaye ni raia wa Uholanzi, Jeremie Frimpong, mwenye umri wa miaka 23, anavutiwa na Liverpool katika hatua ambayo inaweza kumfanya Trent Alexander-Arnold kuhamia katikati ya uwanja. ***(Football Insider)***

### UTD YAIGOMEA NEWCASTLE

KLABU ya Manchester United bado haijakubali mkataba wa fidia na Newcastle United kwa ajili ya Dan Ashworth na huenda ikalazimika kusubiri miezi kadhaa kabla ya kumteua kama mkurugenzi wao wa michezo. ***(Guardian)***

### DIAZ AWAVURUGA VIGOGO

KLABU ya Paris St-Germain na Barcelona zinavutiwa na mshambuliaji wa Liverpool, Luis Diaz, ambaye wakala wake alimtembelea mchezaji huyo wa kimataifa wa Colombia mwenye umri wa miaka 27 hivi karibunii. ***(Telegraph)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# ANCELOTTI: TUNAWEZA KUWAFUNGA CITY KWAO

## ●●● Kocha huyo anaipa nafasi Madrid kusonga mbele endapo...

**MADRID,** Hispania

CARLO Ancelotti ametabiri kitu kizuri kwa Real Madrid kutinga hatua ya nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, akisema watajaribu kurudia kiwango kilichowafanya watoke sare ya mabao 3-3 dhidi ya Manchester City katika mechi ya mkondo wa pili itakayochezwa Aprili 17, mwaka huu.

**Katika mchezo huo wa robo fainali ya kwanza, Bernardo Silva aliiweka City mbele mapema kwenye Uwanja wa Santiago Bernabeu, kabla ya Ruben Dias kujifunga na Rodrygo awaweka mbele Madrid hadi mapumziko.**

Phil Foden na Josko Gvardiol kila mmoja alifunga bao na kuiweka City mbele, kabla ya Fede Valverde kufanya mabao kuwa 3-3 na mchezo kumalizika kwa sare.

"Tulitaka kuchukua faida kidogo, lakini tunapaswa kuridhika, kwa sababu tulishindana," alisema Ancelotti akiiambia Movistar.

"Ikiwa tutafanya hivyo kule Manchester kitakuwa kitu kizuri."

"Mradi tu tulikuwa na nguvu ya kushinikiza juu na kuwafanya wasistarehe, tulifanya vyema," aliongeza wakati akizungumza katika mkutano wake na waandishi wa habari baada ya mechi hiyo.

"Tulianza vibaya tukaruhusu goli, lakini timu ikaanza kucheza, kushinda mpira na kutafuta mabadiliko, walifunga mabao mawili makubwa, lakini sisi tulikuwa na dhamira ya kurejea mchezoni.

"Ilikuwa ni mchezo ambao tungeshinda. Tulikuwa na nafasi ya kufanya matokeo kuwa 3-1. Lakini tungeweza kupoteza pia. Tunapaswa kucheza mchezo kwa kiwango kile kule Manchester na tuone kitakachotokea."

Katika nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa msimu uliopita, Madrid na City zilitoka sare ya 1-1 katika mechi ya kwanza iliyochezwa Bernabeu kabla ya ushindi mnono wa mabao 4-0 waliopata City kwenye mkondo wa pili na kutinga fainali.

"Tofauti na mchezo wa mwaka jana, wazo ni kwenda nao kidole kwa miguu kama tulivyofanya leo (juzi), na kuona nini kitatokea," aliongeza Ancelotti.

"Kutoka kwa upande wetu, tumeridhishwa na tulichofanya na tunatumani kurudia hivyo kule Manchester."

Kocha wa City, Pep Guardiola alikosoa hali ya uwanja wa Bernabeu, na kazi ya ujenzi katika uwanja huo uliojengwa upya bado unaendelea.

"Uwanja ni wa kuvutia," aliiambia Movistar. "Sasa wanapaswa kutunza nyasi. Ni lazima waimarishe hali hiyo. (Rais wa Madrid) Florentino Perez inabidi tu kuwa na wasiwasi kuhusu uwanja mzuri, kama Madrid imekuwa nayo siku zote."

"Ni kile wachezaji wangu walisema," aliongeza Guardiola alipoulizwa kuhusu maoni katika mkutano wake na waandishi wa habari.

"Lakini watu wasichukulie vibaya, uwanja ni wa kuvutia. Nilipocheza, Madrid ilikuwa na uwanja wa ajabu, ulikuwa kama zulia, na sasa haiko hivyo. Lakini nina uhakika watairekebisha."




# TUCHEL ALIA KUNYIMWA PENALTI

**LONDON,** England

KOCHA wa Bayern Munich, Thomas Tuchel, ameelezea kukerwa kwake na mwamuzi raia wa Sweden, Glenn Nyberg, kushindwa kutoa penalti kwa "kosa la kitoto" wakati wa mechi ya mkondo wa kwanza wa robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Arsenal iliyochezwa juzi usiku.

Miamba hao wa Bundesliga walipata sare ya 2-2 kwenye Uwanja wa Emirates huku Bukayo Saka akiifungia timu ya nyumbani dakika ya 12 kabla ya Serge Gnabry kusawazisha dakika ya 18 na penalti wa Harry Kane ikawaweka Bayern Munich mbele hadi mapumziko.

Mchezaji wa akiba Leandro Trossard alisawazishia Arsenal dakika ya 14 kabla ya mchezo kumalizika na Saka alihisi angefaa kupata penalti dakika za lala salama alipodondoshwa na kipa wa Bayern Munich, Manuel Neuer.

Lakini Tuchel alizungumzia uamuzi wa dakika ya 66, matokeo yakiwa 2-1 kwa Bayern Munich, David Raya alipocheza mpira uliopigwa na Gabriel na mlinzi wa Arsenal akauchukua mpira kwa mikono yake kabla ya kujaribu kuanza tena mchezo ingawa mpira ulikuwa unaendelea.

Bayern Munich walipinga lakini hawakupewa chochote.

"Kwangu, kwa sisi sote, alifanya makosa makubwa kutotoa penalti ya mpira wa mikono," alisema Tuchel akiwaambia waandishi wa habari.

"Najua ni hali ya mambo, lakini wanaweka mpira chini, anapiga filimbi, anatoa mpira na beki anachukua mpira mkononi.

"Kinachotukera sana ni maelezo ya uwanjani, aliwaambia wachezaji wetu ni kosa la mtoto na hatatoa penalti ya namna hii kwenye robo fainali, haya ni maelezo ya kutisha, anahukumu mpira wa mikono. Kosa la mtoto, kosa la mtu mzima.

Arteta alikataa kuhusishwa na changamoto ya Saka -- ambayo ilimwacha winga huyo akiwa na hasira kwa muda wote.

"Sijaiona," alisema. "Uamuzi unafanywa. Hatuwezi kubadilisha hilo. Tunapaswa kuzingatia vipengele vingine ambavyo tunaweza kudhibiti. Tungefanya vyema zaidi usiku wa leo (juzi).

## Nyota ya Mainoo yafunguka Manchester Utd

**MANCHESTER,** England

GWIJI wa Manchester United, Nemanja Vidic, amemlinganisha kiungo wa kati wa timu hiyo, Kobbie Mainoo, mwenye umri wa miaka 18 na nyota wa Real Madrid, Luka Modric.


Beki huyo wa zamani wa Mashetani Wekundu, Vidic alihakikisha kumsifu chipukizi huyo baada ya sare ya mabao 2-2 dhidi ya Liverpool katika mechi ya Ligi Kuu England iliyochezwa kwenye Uwanja wa Old Trafford juzi, ambapo Mainoo alifunga bao lake la kwanza kwa timu ya wakubwa nyumbani.

Bao lake la kuvutia katikati mwa kipindi cha pili liliifanya United kuwa mbele kwa magoli 2-1, na hivyo kubadilisha mchezo baada ya kutoka nyuma kwa bao 1-0.

Mainoo tayari amevutia sifa kutoka kwa nyota mbalimbali wa zamani, huku Vidic akiwa ndiye wa hivi punde kusema vyema kuhusu nyota huyo.

Akizungumza na Premier League Productions, Vidic alisema: "Mainoo amekuwa mzuri, haswa ufahamu wake katika maeneo. Ananikumbusha wakati mwingine juu ya Modric.

"Daima anahisi ni nani aliye nyuma yake. Unaweza kuona, alichukua mguso wa kwanza, mara moja akasogea kando na kujipanga."






# Thamani ya Luis Diaz yaanikwa

**LIVERPOOL,** England

LIVERPOOL inamthamini winga, Luis Diaz kwa takriban pauni milioni 75 inapojiandaa kufanya uamuzi kuhusu mustakabali wa mchezaji huyo wa kimataifa wa Colombia msimu huu wa joto, ripoti imesema.

Diaz amebakiwa na masharti yale yale aliyokubali alipojiunga na klabu hiyo kwa mara ya kwanza mwaka 2022, licha ya kufurahia miaka miwili ya kwanza hapo Anfield.

Ingawa mkataba wake uliopo bado utabakiwa na miaka mitatu kukamilika msimu wa joto, gazeti la Telegraph limeema kuwa uamuzi utafanywa kuhusu kuendelea kwa Diaz katika klabu hiyo msimu huu wa joto, huku mkataba mpya na mauzo yakionekana kama uwezekano wakati huu.

Kama klabu nyingine Ulaya, Liverpool wanazidi kufahamu hitaji la kuuza wachezaji kwa wakati mzuri zaidi ili kupata fedha nyingi iwezekanavyo ili kufuata sheria za kifedha, na wanataka kufanya hivyo kwa Diaz.

Liverpool kwa sasa wamemtaja Diaz ana thamani ya pauni milioni 75 - bei ambayo itashuka tu kadiri mkataba uliopo wa mchezaji huyo wa miaka 27 unavyopungua. Barcelona na Paris Saint-Germain zimeonyesha nia ya kutaka huduma ya nyota huyo.

PSG inamwona Diaz kama mbadala wa Kylian Mbappe anayekwenda Real Madrid na haitakuwa na shida kutimiza matakwa ya Liverpool, wakati Barcelona ambao hawana fedha hawawezi kulipa kiasi kama hicho kwa mchezaji yeyote.

Diaz yupo chini ya wakala mmoja na Kocha wa Sporting CP, Ruben Amorim, ambaye ni miongoni mwa walengwa wakuu wa Liverpool kuchukua nafasi ya Jurgen Klopp mwishoni mwa msimu.

Wakala wa Diaz, Raul Costa, alimtembelea winga huyo hivi majuzi huko Merseyside, ingawa madhumuni ya ziara yake hayajafahamika.

## Yanga, Aziz Ki kitaeleweka

INATOKA UKURASA 24

tunafanya vizuri katika michuano ya kimataifa kwa msimu ujao, baada ya msimu huu kuondolewa katika hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, msimu ujao tunahitaji kuvuka hapa," kiliongeza chanzo chetu.

Naye Hersi alipoulizwa kuhusu kuwapo kwa mchakato huo, Rais huyo alikiri Yanga iko katika mpango wa kufanya maboresho ya kuwaongeza mikataba wachezaji ambao mikataba ya sasa inaelekea mwishoni.

"Tunawapa mikataba mipya wachezaji wetu wote imara walioko ndani ya kikosi cha Yanga kwa ajili ya kuendelea nao katika msimu ujao," Hersi alisema.

Hersi aliongeza Yanga haina mpango wala mawazo ya kuuza mchezaji na wanajipanga kumalizana na baadhi ya wachezaji ambao wako mwenye mipango ya benchi la ufundi.

"Kila msimu tumekuwa na mipango yetu, msimu uliopita tulifika fainali ya Kombe la Shirikisho, msimu huu tumeondolewa robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, sasa tunaenda kujipanga kwa kuendelea kuimarisha kikosi chetu kwa ajili ya msimu ujao ili kufikia malengo yetu," aliongeza Hersi.

## Uchovu, ubutu siri Simba SC

INATOKA UKURASA 24

wametekeleza kwa usahihi maagizo aliyowapa na kuibuka na ushindi katika mechi hiyo.

"Ilikuwa mechi nzuri sana kwetu, yale ambayo wachezaji wangu nimewaagiza wameyatekeleza kwa asilimia 75. Tulijua Simba wanacheza mpira wa chini, na kwa sababu wametoka katika michuano ya kimataifa watakuwa 'moto', na mchezaji wetu mmoja (Said Makapu), akatolewa kwa kadi nyekundu, tulichofanya ni mabadiliko ya wachezaji ambao tuliwatuma nini waende wakafanye ili kuziba yale mapungufu.

Tuliongeza namba ya wachezaji nyuma, na walikuwa warefu kwa kazi moja tu ya kupiga vichwa mipira yote ya krosi ambazo wachezaji walikuwa wanategemea, na matokeo yake tumewadhibiti," alisema kocha huyo.

Hii ni mara ya pili kwa Simba kuondolewa na Mashujaa katika mashindano ya Kombe la FA, ilikuwa ni Desemba 26, mwaka 2018 kwenye Uwanja wa Banjamin Mkapa, Wekundu wa Msimbazi ilifungwa mabao 3-2, katika mechi ya raundi ya tatu, wakati huo ikiwa inashiriki Ligi Daraja la Kwanza (sasa Ligi ya Championship).

# MBIVU, MBICHI KENGOLD, PAMBA FC SASA APRILI 28

**Na Adam Fungamwango**

TIMU mbili zitakazopanda daraja moja kwa moja kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao na zile zitakazokwenda kucheza mechi za mchujo zitajulikana rasmi Aprili 28, mwaka huu wakati wa Ligi ya Championship itakapofikia tamati.

Kwa mujibu wa ratiba iliyotolewa na Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), inaonyesha zimebaki mechi tatu kwa kila timu ili kumaliza msimu huku timu mbili zinazotarajiwa kushuka daraja moja kwa moja, pia zitajulikana siku hiyo.

**Hata hivyo, kutokana na msimamo ilivyo, huenda pia baadhi ya timu zitakazopanda Ligi Kuu Bara na kushuka zinaweza kuanza kujulikana baada ya michezo miwili ijayo.**

KenGold inayoongoza katika msimamo wa ligi hiyo ikiwa na pointi 61, inahitaji pointi tano tu ili kufikisha pointi 66 ambazo zitafikiwa na Pamba FC pekee, hivyo inaweza kujihakikishia kupanda daraja endapo itakusanya pointi hizo.


Kwa mujibu wa ratiba hiyo, KenGold imebakisha mechi zake dhidi ya TMA kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid, Arusha itachezwa Aprili 13, mwaka huu itakuwa nyumbani Aprili 21, Uwanja wa Sokoine, Mbeya dhidi ya FGA Talents na mechi ya mwisho Aprili 28, mwaka huu itamaliza dhidi ya Polisi Tanzania kwenye uwanja huo huo.

Pamba iliyo nafasi ya pili ina pointi 58, imebakisha mechi zake dhidi ya FGA Talents (Uwanja wa Nyamagana, Mwanza), dhidi ya TMA (Uwanja wa Black Rhino, Arusha) na Aprili 21 dhidi ya majirani Mbuni FC kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid, jijini Arusha ambayo itafunga pazia.

Biashara United ambayo ipo nafasi ya tatu ikiwa na pointi 56, itacheza nyumbani dhidi ya Green Warriors halafu itaenda ugenini kuivaa Pan African na baadaye kumalizana na Cosmopolitan, huku Mbeya Kwanza ikiwa nafasi ya nne kwa pointi 56 pia, ikiwa imebakisha mechi zake tarehe hizo hizo, dhidi ya Pan African, Green Warriors, na Transit Camp, zote ikichezea nyumbani, Nangwanda Sijaona.



Straika wa Simba, Kibu Denis (katikati), akijipanga kuwatoka nyota wa Mashujaa FC katika mechi ya hatua ya 16 Bora ya mashindano ya Kombe la FA iliyochezwa kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika, Kigoma juzi. Simba iliondolewa katika michuano hiyo kwa kufungwa penalti 6-5. **PICHA: SIMBA SC**





# *Kiduku, Singh kumaliza ubishi*

**Na Saada Akida**

BONDIA wa ngumi za kulipwa nchini, Twaha Kiduku, anatarajia kupanda ulingoni leo kuzichapa dhidi ya mpinzani wake, Harpreet Singh, kutoka India katika pambano la "Hatukimbii Hatuogopi " litakalofanyika kwenye Ukumbi wa Tanzanite, Morogoro .

Kuelekea pambano hilo, Kiduku aliliambia gazeti hili jana amefanya maandalizi mazuri na yupo tayari kukabiliana na mpinzani wake.

"Niko tayari kukabiliana na mpinzani wangu, nimejiandaa vizuri kuwapa burudani watu wangu wa Morogoro kwa kumchapa Singh mapema, ikiwezekana TKO," alisema Kiduku.

Naye Singh alisema amekuja Tanzania kupigana na kuipeperusha vyema bendera ya taifa lake kwa kumtwanga Kiduku katika raundi za awali kwa sababu amefanikiwa kumsoma.

"Nimekuja kupigania bendera ya taifa langu, nimejiandaa vizuri, nimefanikiwa kuangalia mapambano ya mpinzani wangu kwa hiyo haitakuwa na kazi kubwa, natarajia kumaliza kazi mapema," alisema Singh.

Kabla ya mabondia hao kupanda ulingoni kutakuwa na mapambano mengine ya utangulizi ambapo Karim Mandonga atapigana na Mada Maugo huku Muddy Pesa akionyeshana ubabe na Hemed Pelembela kwa upande wa wanawake Debora Mwenda atachapana na Samira Kassim.

Michezo
Alhamisi Aprili 11, 2024
Nipashe



Nyota ya Mainoo yafunguka UKURASA 22

# YANGA, AZIZ KI KITAELEWEKA

Na Saada Akida

●●● Uongozi wajipanga kumpa mkataba mpya, wagoma kuuza...

UONGOZI wa mabingwa watetezi na vinara wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga upo katika hatua za mwisho za mazungumzo kwa ajili ya kumpa mkataba mpya kiungo mshambuliaji wake, Stephanie Aziz Ki, imefahamika.

**Yanga inajiandaa kumpa mkataba mpya wa miaka miwili nyota huyo ambaye amekuwa na kiwango kizuri msimu huu licha ya timu yake kuondolewa katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika na Mamelodi Sundwons ya Afrika Kusini.**

Taarifa kutoka Yanga zinasema lengo la kumbakisha nyota huyo Jangwani ni kuhakikisha kikosi kinaendelea kuwa imara na kinatetea taji lake la Ligi Kuu Tanzania Bara na Kombe la FA.

Chanzo chetu kiliongeza hatua ya kumpa mkataba mpya inatokana na baadhi ya klabu za Afrika Kusini ikiwemo Orlando Pirates kuonyesha nia ya kumhitaji mchezaji huyo.

Mamelodi Sundowns pia imetajwa kuhitaji huduma ya Aziz Ki, ambaye bao alilofungwa walipokutana na timu hiyo kwenye mechi ya marudiano lilikataliwa.

"Kuna hatua kubwa tumefikia katika mazungumzo baina ya Yanga na Aziz Ki, tunajua mchango wake ni mkubwa na ni wazi amekuwa na mwendelezo bora katika kikosi cha Yanga katika michezo ya Ligi Kuu Bara na Ligi ya Mabingwa Afrika," kilisema chanzo chetu.

Chanzo hicho kiliongeza tayari mwakilishi wa Orlando Pirates ameshafika nchini na kuanza mazungumzo ya awali na Aziz Ki ambaye mkataba wake wa sasa unafikia tamati ifikapo Juni, mwaka huu.

"Mchakato wa kumbakisha Aziz Ki unasimamiwa na Injinia (Rais wa Yanga, Hersi Said) mwenyewe, ameshafika mbali katika hatua za mazungumzo naye, nafasi ya kubakia Yanga ni kubwa na inaongezwa nguvu na nia ya kubakia klabuni kutoka kwa mchezaji mwenyewe," chanzo hicho kiliongezwa.



Aziz Ki

Kilisema pia Yanga haina nia ya kumuuza mchezaji huyo endapo itapokea ofa kutoka katika klabu nyingine kwa sababu haitaki kupunguza ubora wa timu yao.

"Hatujafikiria kumuuza mchezaji huyo, na suala la Aziz Ki linafanyiwa kazi kwa umakini mkubwa ili kuhakikisha anaendelea kusalia katika timu yetu, mazungumzo yanavyokwenda, tunaamini tutafikia makubaliano na atakubali kusaini mkataba wa miaka miwili.

Malengo yetu ni kuhakikisha

INAENDELEA UKURASA 23

## Uchovu, ubutu siri Simba kuboronga

Na Adam Fungamwango

KOCHA Msaidizi wa Simba, Selemani Matola, amesema uchovu wa kushiriki mechi za mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, kusafiri na ubutu wa mastraika wake ni moja ya sababu zilizopelekea timu yao kutolewa katika mashindano ya Kombe la FA, imeelezwa.

Simba iliondolewa katika michuano ya Kombe la FA hatua ya 16 Bora baada ya kufungwa penalti 6-5 dhidi ya Mashujaa FC, mechi iliyochezwa kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika, Kigoma juzi.

Wekundu wa Msimbazi ambao ni mabingwa wa Ngao ya Jamii, kwa sasa wamebakia kuwania taji la Ligi Kuu Tanzania Bara pekee.

Akizungumza na gazeti hili, Matola alisema timu yao haikucheza vibaya sana katika mechi hiyo, lakini hawakuwa kwenye ubora wao kutokana na uchovu wa mechi mbili ngumu za hatua ya robo fainali dhidi ya Al Ahly ya Misri lakini pia wakisafiri umbali mrefu kutoka Cairo hadi Dar es Salaam na baadaye kwenda Kigoma.

Matola alisema pia mastraika wake na wachezaji wengine walishindwa kuzitendea haki nafasi nzuri walizozipata kufunga mabao.

"Nafikiri dakika 90 tulikuwa wazuri kuliko wao hasa kipindi cha pili baada ya kuwa pungufu, tumetengeneza nafasi lakini tumeshindwa kuzitumia, unajua uchovu umechangia sana sisi kupoteza mechi hii, tumekwenda katika penalti ambayo siku zote haina mwenyewe, tumetoka katika mashindano haya.

Kama nafasi tumezipata sana lakini wachezaji wetu hawakuwa makini, angalia tulipata nafasi tatu Saido na golikipa, hata wachezaji walioingia kipindi cha pili nao walikosa, tumezichezea wenyewe nafasi, mwisho wa siku tumetolewa kwa penalti," alisema Matola.

Kocha wa Mashujaa, Mohamed Abdallah 'Bares', amewapongeza wachezaji wake akisema

INAENDELEA UKURASA 23




Selemani Matola

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >